JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE) 2021

## KISWAHILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2021

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2021**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI ... iv

1.0 UTANGULIZI ... 1

2.0 SEHEMU YA I : KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ... 2
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ... 2
2.2 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ... 2
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu ... 2
2.2.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi ... 7
2.2.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ... 10
2.2.4 Swali la 4: Utumizi wa lugha ... 13
2.3 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA ... 16
2.3.1 Swali la 5: Tafsiri na Ukalimani ... 16
2.3.2 Swali la 6: Utungaji ... 22
2.3.3 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili ... 26
2.3.4 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili ... 30

3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI ... 36
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ... 36
3.2 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI ... 36
3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla ... 36
3.2.2 Swali la 2: Uhuru wa Mtunzi wa kazi za Kifasihi ... 41
3.2.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ... 44
3.2.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi ... 47
3.3 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA ... 51
3.3.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi ... 51
3.3.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi ... 56
3.3.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya ... 61
3.3.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ... 66

4.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ... 72

5.0 HITIMISHO ... 70

6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ... 73

Kiambatisho A ... 72

Kiambatisho B ... 73

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Kidato cha Sita 2021 katika somo la Kiswahili. Taarifa hii inalenga kutoa mrejesho wa ufaulu wa wanafunzi kwa walimu, wazazi, watunga sera na wadau wengine wa elimu kwa ujumla.

Matokeo ya watahiniwa katika mtihani huu ni kipimo kinachoonesha jinsi mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ulivyofanikiwa kuwapa elimu wanafunzi kupitia walimu wao. Taarifa hii inaonesha namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali kwa kutumia maarifa waliyopata katika ngazi ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita.

Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa watahiniwa kwa mwaka 2021 ni asilimia 100. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika skripti umebainisha kuwa, sababu zilizochangia watahiniwa kufaulu vizuri katika mtihani huu katika mada zote ni pamoja na: uelewa wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa, matumizi sahihi ya lugha na alama zote za uandishi, uzingatiaji wa matakwa ya swali, kutoa hoja sahihi zenye mifano thabiti. Vile vile, sababu mbalimbali za watahiniwa kupata ufaulu wa wastani zimeoneshwa ikiwa ni pamoja na kutoa majibu yasiyojisheleza na kutoa hoja chache katika majibu yao.

Hata hivyo, sababu za watahiniwa kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu zimeainishwa ikiwa ni pamoja na kukosa mitririko mzuri katika majibu yao, kutoandika utangulizi na hitimisho katika maswali ya insha, kukosa weledi wa dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili, kuchanganya majina ya mashairi katika kujibu maswali ya ushairi, kunakili maneno wakati wa ufupishaji wa habari na kujibu maswali kinyume na matakwa ya maswali. Sababu zilizooneshwa katika taarifa hii zitawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kupata mbinu bora za kuboresha zaidi ufaulu katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linawashukuru watahini wa somo la Kiswahili, maafisa mitihani na watu wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kidato cha Sita ulifanyika mwezi Mei 2021. Utungaji wa mtihani huu ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili wa Kidato cha Tano na Sita. Somo hili lilikuwa na karatasi mbili za mtihani ambazo ni 121/1 Kiswahili 1 na 121/2 Kiswahili 2.

Mtihani wa 121 Kiswahili 1 ulikuwa na sehemu mbili, A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali manne (4). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 40. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) tu. Kati ya maswali hayo, swali la tano (5) lilikuwa la lazima na sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60. Mada zilizotahiniwa katika mtihani huu ni pamoja na Ufahamu na Ufupisho, Utumizi wa Lugha, Matumizi ya Sarufi, Utungaji, Maendeleo ya Kiswahili na Tafsiri na Ukalimani.

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulikuwa na sehemu mbili, A na B. Sehemu A ilikuwa na alama 40 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4), mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) na swali la tano (5) lilikuwa la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60. Mtihani huu ulitahini mada za Fasihi kwa Ujumla, Maendeleo ya Fasihi Simulizi, Usanifu wa Maandishi na Uhakiki wa kazi za Fasihi Andishi.

Jumla ya watahiniwa 20,864 walifanya mtihani wa Kiswahili. Kati yao wasichana walikuwa 10,325 na wavulana walikuwa 10,539. Kwa ujumla watahiniwa wote waliofanya mtihani huu mwaka 2021 walifaulu kwa kiwango cha asilimia 100. Pamoja na ufaulu mzuri wa jumla, watahiniwa wachache walipata ufaulu wa wastani na hafifu katika baadhi ya maswali. Ufaulu wa watahiniwa katika maswali umegawanyika katika madaraja matatu ambayo ni: ufaulu mzuri unaoanzia asilimia 60 mpaka 100, ufaulu wa wastani unaoanzia asilimia 35 mpaka 59 na ufaulu hafifu unaoanzia asilimia 0 mpaka 34. Aidha, chati za viwango vya ufaulu kiasilimia zimeambatanishwa mwishoni mwa taarifa hii.

Taarifa hii pia imechambua jinsi watahiniwa walivyojibu kila swali. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa kama vielelezo vya majibu halisi ya watahiniwa.

## 2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

Uchambuzi wa takwimu kwa kila swali umefanyika ambapo ufaulu kwa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ufaulu wa kiwango kizuri, kiwango cha wastani na kiwango hafifu. Sehemu hii itatathmini na kuchambua majibu ya watahiniwa katika mada mbalimbali.

### 2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika karatasi ya kwanza ya somo hili umegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi zaidi ulikuwa kama ilivyooneshwa katika sehemu zifuatazo:

**SEHEMU A**


Sehemu hii ilikuwa na maswali manne, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Kila swali lilikuwa na alama kumi (10).

#### 2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ndogo ya Ufahamu wa Kusoma na Ufupisho na lilikuwa mahususi katika kupima uelewa wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyohusiana na habari aliyoisoma. Swali lilikuwa na vipengele vinne, (a) **-** (d) vyenye jumla ya alama 10.


Kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kutoa maana za maneno aliyopewa; (i) Umevuma (ii) Zama (iii) Kujishaua (iv) Kubweteka (v) Shauku na (vi) Bashasha. Katika kipengele (b) mtahiniwa alitakiwa kufafanua wazo kuu la mwandishi katika aya ya pili, kipengele (c) kilimtaka mtahiniwa kutumia aya moja kueleza athari za ufisadi kwa jamii. Kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kufupisha habari aliyopewa kwa maneno mia moja (100).

Jumla ya watahiniwa 20,864 walijibu swali hili. Asilimia 99.5, sawa na watahiniwa 20,752 walijibu vizuri swali hili na walipata ufaulu wa wastani hadi mzuri kuanzia alama 3.5 hadi 10. Chati Na. 1 inaonesha mchanganuo wa ufaulu katika swali hili.




**Chati Na.1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Watahiniwa 18,626 sawa na asilimia 89.3 walipata alama kuanzia 6 mpaka 10. Watahiniwa 5,454 sawa na asilimia 26.1 walipata alama za juu kuanzia 8 mpaka 10. Watahiniwa hao waliweza kutoa maana sahihi katika vipengele vingi vya maneno waliyopewa, walifafanua vizuri wazo kuu la mwandishi katika aya ya pili, walieleza athari za ufisadi katika jamii na walifupisha habari waliyopewa kwa maneno mia moja (100) kwa kuzingatia hatua za ufupisho. Hata hivyo, viwango vya ufaulu wa watahiniwa vilipishana kwa sababu mbalimbali kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliweza kutoa majibu sahihi katika vipengele (a) – (c) lakini walishindwa kufupisha habari katika kipengele (d), wengine walitoa maana za maneno ambazo hazikutosheleza. Baadhi ya watahiniwa waliweza kujibu kwa usahihi katika vipengele vyote (a) hadi (d). Ufaulu huu unaonesha kuwa watahiniwa walisoma kifungu cha habari na walikielewa vyema hivyo, waliweza kujibu na kupata ufaulu mzuri. Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama nzuri kwa kutoa majibu sahihi kwa vipengele (a) mpaka (d).


01 (a) (i) Umevuma
Maana: Kusifika kwa kitu fulani/Kuenea kwa sifa juu ya jambo fulani.

(ii) Zama.
Maana: Kipindi cha Mwezi; Mwaka au karne.

(iii) Kujishaua.
Maana: Kuringa juu ya jambo/Kujisikia

(iv) Kubweteka
Maana: Kukaa kizembe/Kukaa kimya bila kufanya chochote. (bila kufanya kazi)

(v) Shauku.
Maana: Hamu ya kutaka kujua au kuona jambo.

(vi) Bashasha
Maana: furaha dhidi ya jambo fulani.

(b) Wazo kuu la Mwandishi ni kupambana dhidi ya ufisadi nchini kwani huweza kukwamisha Maendeleo.

**Kielelezo Na.1.1**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Vile vile, uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 2,126 sawa na asilimia 10.2 walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu ulikuwa wa wastani kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwa baadhi ya vipengele. Baadhi ya watahiniwa walitoa maana hafifu za maneno katika vipengele (a) (i) hadi (vi), wengine walitoa kwa usahihi wazo kuu la mwandishi katika kipengele (b). Aidha, watahiniwa wengine waliweza kueleza athari za ufisadi katika kipengele (c), wengine walishindwa kabisa kufupisha kifungu cha habari walichopewa katika kipengele (d) kutokana na kukosa ujuzi wa hatua za ufupisho. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa kwa usahihi baadhi ya maana ya maneno aliyopewa katika kipengele (a) vipengele vidogo kama vile: (i) *Umevuma – kuzungumziwa na watu wengi, (ii) Zama – wakati,* lakini akatoa majibu yasiyo sahihi katika baadhi ya kipengele kama vile: (iii) *kujishaua – ina maana ya kuzembea katika kufanya kitu mfano kufanya kazi kulingana na habari au kifungu cha habari* badala ya kutoa maana sahihi ambayo ni *kuwa na maringo*. Katika kipengele (b), mtahiniwa huyu

aliweza kutoa wazo kuu la mwandishi katika aya ya pili kuwa *mafisadi wamebaini nia ya watanzania ya kutokomeza ufisadi hivyo mafisadi wameacha kujishaua*. Uchambuzi umeonesha kuwa, katika kipengele (d), mtahiniwa alishindwa kabisa kufupisha habari aliyopewa hivyo alipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 112 sawa na asilimia 0.5 walipata alama hafifu kuanzia 0 mpaka 3 kutokana na sababu mbalimbali, kama vile: kushindwa kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi, wengine walitoa maana hafifu za maneno katika kipengele (a) (i) hadi (vi), baadhi walishindwa kutoa wazo kuu la mwandishi katika kipengele (b), na wengine walishindwa kujibu vipengele vyote vya maswali (a) hadi (d) kutokana na kukosa maarifa. Watahiniwa wachache walishindwa kabisa kufupisha habari katika kipengele (d) hivyo kunakili sentensi kutoka katika kifungu cha habari walichopewa. Kutokana na sababu hizo, ufaulu wa watahiniwa haukuwa sawa kwa watahiniwa wote wa kundi hili. Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.

1. (a) Maana ya Maneno yafuatayo ni

(i) Umevuma - lina maana ya kuwa kitu - kuenea kwa sana Mfano kutokana na - habari juu ya Mafisadi kuwa "Ufisadi Umevuma" au Umeenea.

1(a) (ii) Zama - likiwa na Maana ya nyakati au wakati kulingana na lilivyotumika katika - kifungu cha habari

(iii) Kujishaua - lina maana ya kuzembea katika kufanya kitu mfano kufanya kazi kulingana na habari au kifungu cha habari.


(iv) Kubweteka - lina maana ya kuridhika au kupotezea kulingana na hali Mfano kulingana na kifungu cha habari juu ya Ufisadi "Watanzania hawako tayari kubweteka - na kelele za Mafisadi.

(v) Shauku - likiwa na Maana ya hamu na matamanio Mfano kulingana na kifungu cha habari juu ya kupiga vita - ufisadi Watanzania wana hamu na kuona Mafisadi wanachukuliwa hatua.

(vi) Bashasha - kumanisha hamasa na ari juu ya jambo fulani Mfano katika kifungu cha habari inasema.

"Watanzania wana bashasha ya kuona - mabadiliko yanayoshinikizwa na nchi juu ya Ufisadi"

(b) Wazo kuu la Mwandishi katika aya ya pili ni juu ya UMUHIMU WA UADILIFU KATIKA KAZI


1 (c) Kwa aya moja zifuatazo ni athari za Ufisadi kwa jamii

Ufisadi katika jamii huweza kuwa na athari kama vile kudidimiza uchumi wa taifa, kugandamiza haki za Mwanadamu, kuchochea kuibuka kwa Matabaka katika jamii, dhuruma na Unyanyasaji, migogoro katika jamii na kulikosesha taifa fedha za kigeni katika kuleta mafanikio.

(d) Ufupisho wa habari kwa maneno mia moja kama ifuatavyo

Licha ya kuwa Ufisadi umekuwa kama wimbo katika jamii ya Tanzania, pongezi ziwafikie pia watanzania wenyewe kwa kuwa tayari kuunga mkono juhudi za serikali dhidi ya hujuma ya Ufisadi katika jamii yetu ya Tanzania kwani watanzania wamekuwa na shauku kubwa sana na ari ya kutaka kuwaondosha viongozi wasio adilifu kazini

Hakika serikali ichukue njia sahihi za kuondosha watu wasiopenda kutetea maslahi ya taifa letu kwani taifa huingia hasara kwa kukosa maendeleo katika nyanja zote za kimaisha ikiwemo kijamii, kiuchumi na kisiasa -


**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu Swali la 1

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefupisha kifungu cha habari tofauti na alichotakiwa kufupisha.

### 2.1.2 Swali la 2: Matumizi ya Sarufi


Swali hili lilitoka katika mada ya Matumizi ya Sarufi katika mada ndogo ya Aina za Maneno. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lililenga kupima utumizi. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha dhima nne za kielezi katika lugha ya Kiswahili.

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 20,864 walijibu swali hili. Kati yao, asilimia 83.3, sawa na watahiniwa 17,372 walijibu vizuri swali hili na walikuwa na ufaulu wa wastani hadi mzuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 mpaka 10. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*


Watahiniwa 13,207 sawa na asilimia 63.3 waliweza kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama kuanzia 6 mpaka 10. Kati yao, asilimia 31.9 walipata alama nzuri kuanzia 8 hadi 10. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kutokana na sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa waliweza kubainisha dhima tatu za kielezi katika lugha ya Kiswahili mfano, *kuonyesha namna tendo lilivyofanyika*, *kuonyesha wakati* na *kuonyesha idadi* na kutoa mifano kwa kila dhima kwa kubainisha vielezi katika sentensi zao. Watahiniwa wengine walitaja dhima nne za kielezi lakini walitoa mifano kwa baadhi tu ya dhima, lakini wapo na wengine waliotoa na kufafanua kwa usahihi dhima zote za kielezi katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na tofauti za ubora wa majibu ya watahiniwa katika kundi hili walipata alama tofauti tofauti Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha dhima nne za kielezi katika lugha ya Kiswahili.


2. Dhima za kielezi
(i) Kuonyesha mahali
mfano. Mwalimu ameingia darasani
E
(ii) Kuonyesha jinsi au namna tendo linafanyika
mfano: Nasma anaongea taratibu
E
(iii) Kuonyesha idadi
mfano: Cherij huwa anaimba kila siku
E
(iv) Kuonyesha wakati.
mfano: ~~AA~~
Mwanalusi alitoroka juzi usiku
E.

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 4,165 sawa na asilimia 20 walipata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5. Ufaulu wa wastani wa watahiniwa ulitokana na sababu zifuatazo: baadhi waliandika kwa usahihi baadhi ya dhima za kielezi, lakini walishindwa kuandika dhima nyingine. Wengine walichanganya dhima za kielezi na aina ya kielezi. Wengi walitoa maana na sifa za kielezi na wengine walitoa dhima za kielezi bila kuzitolea ufafanuzi kutokana na kukosa ujuzi wa mada ya aina za maneno. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa dhima sahihi za kielezi, kama vile: *kueleza jinsi tendo linavyofanyika mfano Khamis anakula kidogokidogo, kueleza wakati tendo linapofanyika mfano wazee walitembea usiku kucha.* Lakini, alitoa dhima za kielezi zisizo sahihi kama vile: *huburudisha, hukosoa* na *huelimisha.* Hivyo, ufaulu wa watahiniwa katika kundi hili haukulingana japokuwa wote walikuwa na alama za wastani.

Watahiniwa 3,492 sawa na asilimia 16.7 walipata alama hafifu kuanzia 0 mpaka 3 kutokana na sababu zifuatazo: wapo waliotoa dhima moja ya kielezi. Wengine walitoa sifa za kielezi badala ya kubainisha dhima za kielezi, huku wengine wakishindwa kabisa kubainisha dhima nne za kielezi na mifano yake kutokana na kukosa ujuzi katika dhima za vielezi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja aina za vielezi kama vile: *vielezi vya wakati, vielezi vya namna/ jinsi, vielezi vya mahali* na *vielezi vya idadi* bila kutoa ufafanuzi, kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.



2. Bainisha dhima nne za kielezi katika lugha ya kiswahili

Kielezi; Ni ile njia ya kutoa maelezo marefu au mafupi ili kuweza kupata maana kamili ya ujumbe, neno au jambo. katika maisha ya binadamu kujieleza ni jambo la muhimu sana.

Zifuatazo ni dhima za kielezi katika lugha ya kiswahili:

Huelewesha; kielezi kina dhima ya ~~kielezi~~. kuelewesha - Hapa ni pale ambapo mtu au kitu kina elezewa kwa kawaida au kwa ufasaha ili mtu aweze kuelewa.

Huondoa utata; kielezi katika lugha kinasaidia kuondoa kutokana pale ambapo kuna maelezo kuna kua na uelewa mkubwa na mtu anayetumia lugha ya kiswahili hatapita tabu ya kuelewa mfano. Mama yake juma anampenda sana mwanae amemnunulia zawadi. Sana ni kielezi.

Kielezi kinapulisha; Hii ni ile hali ya kuelezea au kutumia kielezi cha lugha ya kiswahili kuelezea jambo fulani. Hupulisha mtu au kitu kimetendeka je mfano. Tanzania ilipata Uhuru mwaka 1961 kutoka kwenye Ukoloni. Ilipata ni kielezi cha kupulisha.

Kielezi huhamasisha; kielezi katika lugha ya kiswahili hua kina hamasisha; Hii ni kwa sababu husaidia kueleza na kumfanya mtu kubadili mwenendo wake. Mfano Ukisoma kwa bidii utafaulu. kielezi hapo ni Ukisoma kwa bidii na vilevile. kufaulu kuna hamasisha.

mwisho; kielezi katika lugha ya kiswahili kina dhima nyingi sana ambazo husaidia lugha kuku


**Kielelezo Na. 2.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama hafifu.

Kielelezo Na, 2.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa yasiyoendana na dhima za kielezi.

### 2.1.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi


Swali lilitoka katika Mada ya Matumizi ya Sarufi, mada ndogo ya Matumizi ya Mofimu, Matawi ya Sarufi na Ufafanuzi wa Tungo. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lililenga kupima kumbukumbu. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza dhana za kisarufi alizopewa kwa kutumia mifano.

Swali hili lilifanywa na watahiniwa wote 20,864. Miongoni mwao watahiniwa 17,289 sawa na asilimia 82.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Watahiniwa 11,363 sawa na asilimia 54.5 walifanya vizuri swali hili kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, watahiniwa 4,525 sawa na asilimia 21.7 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 8 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa dhana za kisarufi walizopewa pamoja na kuzitolea mifano yake. Watahiniwa wengine walishindwa kutoa maana toshelevu kwa baadhi ya dhana za kisarufi walizopewa kwa mfano, walielezea dhana ya (e) *alomofu* kwa kuifananisha na *mofu*, lakini wachache waliweza kueleza kwa usahihi dhana zote kuanzia (a) hadi (e) na kuzitolea mifano. Hivyo, ufaulu wa watahiniwa wa kundi hili haukulingana. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza dhana za kisarufi kwa usahihi na kutoa mifano kwa kila kipengele kama vile; kipengele *(a) mofolojia –hujishughulisha na uchambuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofimu mbalimbali ili kuunda maneno mfano, anacheza (b) mzizi huru –mzizi wa neno unaweza kusimama pekee na ukaleta maana (c) viambishi – ni vipashio vinavyopachikwa kabla au baada ya mzizi wa neno mfano chez-a, (d) sentensi sahili –inatoa taarifa kamili, mfano, Mwalimu anafundisha*, na *(e) Alomofu – maumbo tofauti ya mofimu moja mfano mw-, m-, mu-, ni maumbo yanayowakilisha mofimu ya idadi ya umoja*. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.



3. (a) Mzizi huru ni aina ya mzizi ambao unaweza kusimama pekeake na kutumika kama neno kamili, bila kuongezwa viambishi vyovyote mfano Baba, bibi, sungura, mama na kaka

(b) Mofolojia ni tawi la sarufi linalojishughulisha na jinsi au namna maneno yanavyoundwa ~~mfano~~, kipashio cha mingi kabisa cha kimofolojia ni mofu ambalo ni umbo la neno linalowakilisha mofimu ambalo hudhihirika kiothografia na kifonolojia mfano baba, mama (mofu huru) na mofu tata kama ile katika kitenzi Alimpigia, a-li-m-pig-i-a mofu -i- ni mofu tata - yenye maana zaidi ya moja yaani kitumizi, namna au badala ya

(c) Viambishi ni vipashio ~~mofu~~ vinavyopachikwa mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa neno ili kuunda neno kamili mfano neno Anacheza, A-na-chez-a, A-na ni viambishi awali vilivyopachikwa katika mzizi wa -chez- na -a ni kiambishi tamati kilichopachikwa katika mzizi wa -chez-.


(d) Sentensi sahili ni aina ya sentensi ambayo inajitosheleza na imeundwa na kiima na kiarifu mfano Mama anapika. hii ni sentensi sahili

(e) Alomofu ni maumbo kadhaa tofauti tofauti yanayotumika kuwakilisha mofimu moja mfano Mw, Mu na m katika muktadha wa Mwalimu, Muuguzi na mtoto ambapo maumbo mw, mu na m ni alomofu za mofimu moja ya kuonyesha idadi ya umoja

**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Watahiniwa 5,926 sawa na asilimia 28.4 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Baadhi yao walitoa majibu sahihi katika vipengele (b), (d) na (e) na majibu yasiyo sahihi kwa vipengele vingine, kwa mfano: (a) mzizi huru *ni neno lenye shina* na (c) viambishi *ni fonimu zenye maana*. Watahiniwa wengine hawakujibu kabisa baadhi ya dhana walizopewa hasa kipengele (e) kutokana na kukosa maarifa juu ya alomofu. Aidha, kuna baadhi ya watahiniwa ambao walitoa maana ya dhana ya mzizi ambayo haikuwepo kwenye swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana sahihi ya mzizi wa neno kuwa ni *sehemu ya neno inayobakia baada ya kuondoa viambishi vyote*, alomofu ni *maumbo mbalimbali yanayowakilisha mofimu moja*. Hata hivyo, mtahiniwa alishindwa kabisa kutoa maana ya mofolojia na sentensi sahili. Majibu ya watahiniwa hao yanadhihirisha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana zilizopimwa.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, jumla ya watahiniwa 3,575 sawa na asilimia 17.1 walijibu swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kwa sababu zifuatazo: wote hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana za kisarufi walizoulizwa, wengine walieleza dhana ya *alomofu* kwa kuichanganya na dhana ya mofu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa, Alomofu ni *aina ya kiambishi cha ngeli za nomino.* Wengine walishindwa kabisa kufafanua hata dhana moja ya kisarufi waliyoulizwa, hivyo, walipata alama hafifu. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza na kutoa mifano ya dhana za kisarufi kwa usahihi.


3 a) Mzizi huru
hii ni neno ambalo hua
hii ni shina la neno linaloweza kunyambuliwa
na kubeba na maana ile ile mf: A-na-Soma
b) Mofolojia
hii ni aina ya maneno yenye maana na
mfumo wa kimaandishi moja
c) Viambishi
hii ni aina ya maneno yanayosimama badala
ya nomino Mfano Mwajuma anapika Chakula
d) Sentensi Sahili
Hii ni aina ya Sentensi ambayo huchambuliwa
kwa mhimili wa Sentensi Mfano: Unapo kwenda
msalani unatakiwa uwe na usafi wa hali
ya juu
e) Alomofu
Haya ni maneno yanayo simama kama ya
kisintaksia.


**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Alipata Alama Hafifu

### 2.1.4 Swali la 4: Utumizi wa Lugha

Swali hili lilitoka katika mada ya Utumizi wa Lugha, mada ndogo ya Utata wa Lugha. Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa maana mbili kwa kila sentensi

alizopewa katika vipengele (a) mpaka (e). Swali lilikuwa na jumla alama 10 na lilikuwa mahsusi kupima utumizi.

Watahiniwa 20,864 sawa na asilimia 100 walijibu swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 18,794 sawa na asilimia 90.1 walikuwa na kiwango cha ufaulu cha wastani na kizuri kwa kuwa walipata kuanzia alama 3.5 hadi 10. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swala 4.




**Chati Na. 4**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia 4*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 14,229 sawa na asilimia 68.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 8,145 sawa na asilimia 39 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10 kutokana na sababu zifuatazo: walikuwa na ujuzi wa utata katika lugha, walifanikiwa kutoa maana mbili za sentensi katika vipengele vingi na walishindwa katika vipengele vichache, wengine walitoa maana sahihi katika sentensi zote walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa maana hizo kama vile katika kipengele (a), mwalimu wetu wa kifaransa alitutembelea jana. Maana *(i) mwalimu wetu mwenye asili ya Ufaransa alitutembelea jana (ii) mwalimu wetu wa somo la Kifaransa alitutembelea jana,* (b), Mzee Mangungo aliwachezea sana wanangu. Maana *(i) alicheza kwa niaba ya wanangu (ii) amewaroga wanangu* (c), Mtumishi wake alimuibia gari jipya. Maana *(i) Mtumishi aliiba gari ya kiongozi wake wa kazi (ii) Mtumishi aliiba gari kwa ajili ya kiongozi wake wa kazi* na vipengele (d) na (e) alitoa maana mbili sahihi.

Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

4. a) Mwalimu wetu wa kifaransa alitutembelea jana.
– Mwalimu wetu anayefundisha kifaransa alitutembelea jana.
– Mwalimu wetu anayetoka ufaransa alitutembelea jana.

b) Mzee mangungo amewachezea wanangu.
– Mzee Mangungo amecheza kwa ajili ya wanangu.
– Mzee Mangungo amewaroga wanangu.

4. c) Mtumishi wake alimwibia gari.
– Mtumishi wake aliiba gari kwa ajili yake.
– Mtumishi wake aliiba gari lake.


d) Wizi wa silaha umeongezeka sana siku hizi.
– Wizi wa kuiba silaha umeongezeka sana siku hizi.
– Wizi kwa kutumia silaha umeongezeka sana siku hizi.

e) Yule bibi ni mpangaji mzuri.
– Yule bibi anapanga vitu vizuri.
– Yule bibi anaishi kwenye nyumba anayolipia vizuri.

**Kielelezo Na 4.1**: Sampuli ya Majibu Fasaha ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Watahiniwa 4,565 sawa na asilimia 21.9 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walijibu kwa usahihi baadhi tu ya vipengele vya swali, lakini walishindwa kujibu vipengele vingine. Aidha, baadhi yao walitoa maana zisizotoshelevu na wengine walifanikiwa kujibu vipengele vichache kwa usahihi na kuacha vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa maana mbili katika kipengele *(b) Mzee Mangungo aliwachezea sana wanangu.* Maana *(i) aliwahangaisha na mambo yasiyo na msingi (ii) aliwaroga* na kipengele (e) *Yule bibi ni mpangaji mzuri.* Maana *(i) Yule bibi ana mpangilio mzuri wa vitu vyake (ii) Yule bibi anaishi nyumba anayolipia kodi.* Hta hivyo, mtahiniwa mmoja alishidwa kutoa maana sahihi katika vipengele (a), (c) na (d) kutokana na kukosa misamiati ya lugha ya Kiswahili, hivyo alipata ufaulu wa kiwango cha wastani.

Data katika chati Na. 4 inaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu kuanzia 0 mpaka 3 walikuwa 2,070 sawa na asilimia 9.9. Kwa ujumla watahiniwa hao walikuwa na ufaulu hafifu kwa sababu walikuwa na maarifa madogo kuhusu mada ya utata katika sentensi, kutoa maana mbili za sentensi katika vipengele vichache, wengine kushindwa kabisa kutoa maana mbili katika sentensi na wengi walitoa maana ambazo hazikuendana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kabisa kutoa maana mbili kwa sentensi zote alizopewa kwa mfano, katika kipengele *(a)* *"*mwalimu wetu wa kifaransa alitutembelea jana". Maana mtahiniwa alishindwa kabisa kutoa maana hata moja. Kipengele *(b), "*Mzee Mangungo aliwachezea sana wanangu" mtahiniwa alieleza: *(i) aliwachochea (ii) kawaibia, (c) "*Mtumishi wake alimuibia gari jipya". Mtahiniwa alieleza: *(i) mtumishi ni mwizi (ii) bosi wake ni mwizi (d). "*Wizi wa silaha umeongezeka sana siku hizi". Mtahiniwa alieleza *(i) utapeli umeongezeka (ii) silaha zimezagaa.* Katika kipengele *(e),* mtahiniwa hakuweza kujibu kabisa. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.




**Kielelezo Na 4.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu.


## 2.2 SEHEMU B

Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali manne ya insha. Swali la tano (5) lilikuwa ni la lazima. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu, na kila swali lilikuwa na alama 20.

### 2.2.1 Swali la 5: Tafsiri na Ukalimani

Swali hili lilitoka katika mada ya Tafsiri na Ukalimani, mada ndogo ya Tafsiri na lilikuwa maalum kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua sifa nane za mfasiri bora wa matini.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili lilifanywa na watahiniwa wote 20,864 kwa kuwa lilikuwa la lazima. Watahiniwa 20,219 sawa na asilimia 96.9 walifaulu kwa kiwango cha wastani na kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 19.5. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5.




**Chati Na. 5**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*


Watahiniwa 14,016 sawa na asilimia 55.1 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 19.5. Miongoni mwao, watahiniwa 425 sawa na asilimia 02 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 19.5. Katika majibu yao watahiniwa walionesha sifa stahiki za mfasiri lakini kwa uchache, wengine walitaja sifa zote japokuwa maelezo ya baadhi ya sifa hayakujitosheleza na wachache walitoa sifa za mfasiri na kuzielezea kwa usahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua sifa, kama vile (i) *awe mahiri wa lugha mbili, (ii) awe mwandishi na mhakiki, (iii) awe na marejeo sahihi, (iv) asome machapisho na majarida (v) asomee taaluma ya tafsiri, (vi) asiwe mpondaji wa kazi za waandishi* na *(vii) awe makini na mtenda haki (viii) ajue utamaduni wa lugha zote anazoshughulika nazo*. Utofauti wa ubora wa majibu ya watahiniwa ndiyo uliosababisha alama za watahiniwa kutofautiana. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

5 Mfasiri ni mtu anaye hawilisha mawazo kutoka lugha moja kwenda nyingine yaani kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa nia ya mwandishi pasipo kupoteza Maana iliyo kusudiwa. Kuna aina nne za tafsiri ambazo ni tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri maana. Zifuatazo ni sifa za Mfasiri bora ÷

Ajue lugha mbalimbali, kutokana na kwamba kazi ya kutafsiri inahusisha lugha mbili hivyo ni muhimu mfasiri aweze kujua lugha mbalimbali zitakazo mwezesha kufanya kazi yake ya kutafsiri kwa ufanisi zaidi kwa mfano kama anatafsiri matini ilikatika kiingereza kwenda kiswahili ni lazima ajue kiingereza vizuri pamoja na kiswahili hivyo kufanya kazi yake ya kutafsiri kuwa bora zaidi.

Ajue utamaduni mbalimbali, kutokana na kwamba kazi ya kutafsiri ina husisha lugha mbili tofauti ambayo ni lugha chanzi na lugha lengwa hivyo ni muhimu mfasiri kujua utamaduni wa lugha ambazo anashughulika nazo katika kufanya tafsiri kwani kuna tamaduni mbalimbali katika lugha hivyo ni muhimu kujua tamaduni hizo mfano kwa waingereza wao wana milo miwili tu kwa utamaduni wetu katika kiswahili tuna milo mitatu.

Ajue Matini kwa undani, mfasiri kabla ya kuanza kufanya kazi yake ya kutafsiri ni lazima aijue kwa undani matini ambayo anakwenda kufanyia kazi iliyo katika lugha chanzi kabla ~~kabla~~ ya kupeleka katika


5 Lugha lengwa hii itamfanya mfasiri kufanya kazi yake kwa ufanisi na kwa bora.

Awe na weledi wa kusoma, hapa mfasiri anatakiwa kuwa na ujuzi wa kusoma vizuri maandishi ili aweze kutambua maneno na misamiati mbalimbali iliyotumika katika lugha chanzi ili kuweza kufikisha ujumbe ulio kusudiwa kwa wasomaji bila kupotosha maana.

Awe na taaluma ya tafsiri, kwa kuwa kazi ya kutafsiri ina hitaji kuhawilisha mawazo kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa kwa njia ya maandishi bila ya kupotosha maana iliyo kusudiwa hivyo ni muhimu mfasiri awe na taaluma ya tafsiri ili kufanya kazi yake kuwa bora zaidi.

Ajue uwezo wa wahusika, katika mchakato wa kufanya tafsiri ni muhimu mfasiri ajue vizuri uwezo wa wahusika ambao anawafanyia kazi hiyo ili kazi yake iweze kuwa bora kwani akifanya tafsiri pasipo kujua uwezo wa wahadhira yake anaweza ifikisha ujumbe kazi yake haiweza kufanikiwa vizuri.

Awe Mwaminifu, kutoka na kwamba kazi ya kutafsiri ni sawa na ajira zingine hivyo ni lazima mtafsiri awe Mwaminifu katika kufanya kazi yake kwani anapofanya tafsiri ana-lipwa kutokana na kazi anayo ifanya hivyo awe Mwaminifu asiwe tapeli katika kazi ya kutafsiri pia hata kufanya tafsiri kwa ukweli na uaminifu kama jinsi ilivyo matini ya lugha chanzi pasipo ya kubadili maana anapo kuwa akiipeleka kazi yake katika lugha lengwa.

5 Ajue Mazingira, kutokana na kwamba mfasiri anafanya kazi yake katika mazingira mbalimbali ni muhimu ajue mazingira vizuri yale ambayo anafanyia kazi yake ya kutafsiri ili kuweza kufanya kazi yake kuwa bora zaidi na kuweza kusomwa na watu wengi.


Kwa ujumla, tafsiri ni muhimu sana katika maisha ya jamii kwani kuna faida ambazo zinatokana na kazi ya kutafsiri ambazo ni, ni chanzo cha ajira, husaidia kukuza lugha, husaidia kujifunza lugha mbalimbali, husaidia kujifunza utamaduni pia kukuza msamiati wa lugha yaweza kuwa lugha chanzi au lugha lengwa.

**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa aliyepata Alama za Juu.

Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 6,203 sawa na asilimia 41.8 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5

kutokana na sababu zifuatazo: kuna watahiniwa walifafanua baadhi ya sifa za mfasiri wa matini, wengine walichanganya sifa za mfasiri na sifa za mwanafasihi, mfano, *ajue mazingira yaliyomlea msanii, asome vitabu mbalimbali vya fasihi.* Wachache walitoa sifa za mtanzania badala ya sifa za mfasiri kama inavyoonekana katika jibu la mtahiniwa mmoja aliyefafanua sifa za mfasiri bora kama vile: *(i) asome tafsiri mbalimbali, (ii) aweze kusoma machapisho mbalimbali, (iii) awe na taaluma ya tafsiri, (iv) ajue lugha chanzi na lengwa.* Hata hivyo, mtahiniwa alitoa majibu tofauti kabisa katika vipengele mfano katika kipengele cha *(v) mapaka (vi) alieleza: (v) awe mzaliwa wa Tanzania (vi) awe kabila la Tanzania (vii) ajue lugha ya Kiswahili* na *(viii) ajue kusoma na kuandika.* Kutokana na hilo mtahiniwa alipata ufaulu wa wastani.

Pamoja na hayo, watahiniwa 645 sawa na asilimia 3.1 ya waliofanya swali hili walipata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 6. Ufaulu hafifu wa watahiniwa ulitokana na sababu zifuatazo: baadhi yao walijadili aina za tafsiri na wengine walitoa sifa za mkalimani. Watahiniwa wengine walifafanua sifa chache za mfasiri bora wa matini, wapo waliotoa dhima za fasihi badala ya sifa za mfasiri, kama vile: *(i) kuelimisha jamii, (ii) kuburudisha, (iii) kuonya jamii* na *(iv) kuondoa matabaka.* Majibu haya yalikuwa kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelewa mahitaji ya swali, hivyo kupata alama hafifu.



5 Anuai, ni sifa bora za msafiri yaani
kujipanga kwa kile kitu kwenye safari
yako.
Ifuatavyo ni sifa bora za ~~mf~~ msafiri
wa matini:
Kuandaa Nauli, msafiri
wowote lazima hakikishe amejipang-
anga kwa kuandaa Nauli ya kusafiria
ili aweze kufika vizuri safari yake
Kujua muda atakaosafiri,
ni muhimu kupanga kujua ni muda gani
utasafiri ili ajue ukao aendako atat-
umia muda wa kiasi gani
Kuanda Pesa ya kula njiani,
msafiri wowote lazima haandae pesa
ya kula njiani ili aweze kumudu safari
yake.
Lazima nguo zake ziwe safi,
msafiri ahakikishe nguo zake zipo
smarti ili aweze kusafiri kwani
akiwa mchafu hatakuwa picha nzuri
5 katika jamii.
Lazima ajue madhumuni ya safari
yake, msafiri ni lazima ajue lengo la
safari yako ili aweze kusafiri kama
hana lengo na hiyo safari basi itakuwa
nauli anayotumia ni matumizi mabaya
ya fedha.
Kwa hiyo msafiri sambo
muhimu la kuzingatia ni kwa lazima
ahakikishe anayo pesa ya kutosha
kujikimu na safari yake.


**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 5

Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua mahitaji muhimu ya msafiri badala ya sifa za mfasiri. Kwa kukosa umakini, mtahiniwa aliibua neno msafiri badala ya mfasiri na hivyo kuwasilisha majibu ambayo si ya matakwa ya swali.

### 2.2.2 Swali la 6: Utungaji

Swali hili lilitoka katika mada ya Utungaji, mada ndogo ya Uandishi wa Insha na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika insha yenye maneno mia tatu (300) kuhusu utamaduni wa Tanzania.

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili lilifanywa na watahiniwa 12,159. Watahiniwa 11,933 sawa na asilimia 98.1 walijibu vizuri swali hili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo watahiniwa walikuwa na ufaulu wa wastani na mzuri, na walipata alama kuanzia 6.5 hadi 20. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa 7,732 sawa na asilimia 63.5 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 12 mpaka 20. Kati yao, watahiniwa 213 sawa na asilimia 1.2 walipata alama kuanzia 18 hadi 20. Watahiniwa waliojibu vizuri swali hili walikuwa na uelewa mkubwa kuhusu utamaduni wa Tanzania, hivyo, waliweza kuandika insha kwa kuzingatia: (i) kichwa cha insha kwa herufi kubwa, (ii) utangulizi wa insha, (iii) kiini cha insha kwa kufafanua misingi ya utamaduni, faida za utamaduni, hasara zitokanazo na misingi mibovu isiyozingatia utamaduni wetu, (iv) walitoa hitimisho na (v) matumizi ya lugha fasaha, taratibu za uakifishaji pamoja na kuzingatia idadi ya maneno kwa ufasaha. Aidha, kulikuwa na mpishano wa alama baina ya watahiniwa kwa sababu

kulikuwa na dosari ndogo ndogo katika majibu yao. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika kichwa cha habari kwa herufi ndogo, mfano *"utamaduni wa Tanzania"* lakini sehemu zingine waliandika kwa usahihi. Watahiniwa wengine waliandika insha bila kuweka mapendekezo na hitimisho. Vile vile, wapo ambao hawakuzingatia alama za uandishi, na wachache waliandika kwa kuzingatia hatua zote za uandishi wa insha na hivyo, walipata alama za juu. Kielelezo Na. 6.1 ni majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

6 Insho ya Maneno 300 kuhusu utamaduni wa Tanzania

UTAMADUNI WETU

Utamaduni ni jumla ya mambo yanayofanywa na watu wa jamii fulani kwa kuzingatia mila na desturi kwa kila siku. Utamaduni wa Tanzania unajihusisha na njanja zifuatazo

Kuvaa: Mavazi ya watanzania walowengi ni nguo ndefu na zenye heshima. Japo kuwa tunayo ~~mavy~~ Mavazi Maalumu ya kikabila kwa mfano wamasai huvaa mashuka. katika mkindo wa Lubega.

Kula. Watanzania hawana chakula kimoja japo vipo baadhi ya vyakula ambavyo hutumiwa na makabila yaliyo mengi nchini navyo ni kama Ugali, Makande, ~~Mihogo~~ Mihogo, mboga za Majani na Matunda

Nyimbo na Ngoma: watanzania pia wanazo nyimbo na ngoma za asili mfano wa ngoma hizo ni Mdundiko, Sindimba pia wanao utamaduni wa kuwacheza vijana wao wa kike na kiume wakati wanapokuwa/kubalekhe na hata baada ya kutairiwa yaani Jando na Unyago

Kuabudu. watanzania pia wanazo dini zao ukiacha dini zilizokuja na wazungu ikiwemo Uislamu na Ukristo. Zipo dini zetu za kipagani ambazo tunaabudu miungu yetu (Mizimu) na katika ibada hizo huwa kunatolewa kafara/Sadaka ya wanyama kama Mbuzi, kuku, kondoo ili kufanikisha jambo tuliomba

Miiko, katika tamaduni za kitanzania pia tunayo miiko. Miiko ni makatazo yanayotolewa na baadhi ya wazee au wakubwa waliotutangulia kuzaliwa. Katika miiko kuna ya kiafya Mfano Mama mjamzito kukatazwa kula Mayai ~~kwa~~ kwa jamii ya kimasai na nyingine hii ina maana iwapo atakula Mayai nayo yana protini nyingi itampelekea kujifungua Mtoto Mkubwa na kumsababishia mama wakati mgumu ajifungapo, pia kwa hao wajawazito ~~kwa~~ hawaruhusiwi kula ~~ng~~ Nyanya chungu, pilipili vitapelekea mtoto kuzaliwa

| | |
|---|---|
| 6 | na upele mwilini na macho mekundu mno. |
| | Hivyo basi sisi kama watanzania tudumishe na kue- |
| | nzi mila na desturi zetu katika mavazi tusiwaige wazungu |
| | kuvaa nguo fupi zenye kuonesha au kubana. Pia tudumishe vyaku- |
| | la vyetu kwani vyakula vyetu ndio afya bora kwetu. Mfano ku- |
| | la matunda na mboga za majani zaidi. UTAMADUNI WETU NI |
| | FAHARI YETU SISI WATANZANIA. Tuudumishe tuuenzi na |
| | kuufuata kwani tukijipenda na wengine watatufuata na |
| | kutupenda. ~~pia~~ |

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Aidha, watahiniwa 4,201 sawa na asilimia 34.6 walikuwa na ufaulu wa wastani kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 11.5. Watahiniwa hao waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele. Kwa mfano, waliweza kutoa kichwa cha habari na kutoa maelezo sahihi katika kiini cha insha, lakini walishindwa vipengele vingine, kama vile, maoni na mapendekezo pamoja na hitimisho. Vile vile, baadhi ya watahiniwa waliweza kuandika kichwa sahihi cha insha na kutaja hoja za utamaduni lakini walitoa maelezo hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kichwa cha habari *UTAMADUNI* na akataja vipengele vya utamaduni kama vile *mavazi, ulaji na miiko,* lakini alishindwa kutetea hoja zake na hakutoa mapendekezo wala hitimisho. Tofauti hizo za ubora wa majibu ya watahiniwa zilisababisha kutofautiana kwa alama miongoni mwao.

Ufafanuzi zaidi wa uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 226 sawa na asilimia 1.9 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6. Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu uandishi wa insha. Baadhi ya watahiniwa hawakuandika kichwa cha insha, hawakuzingatia alama za uandishi, wala hawakuwa na hitimisho la insha. Watahiniwa wengine katika kiini walishindwa kueleza hoja za utamaduni wa mtanzania na wachache waliandika insha yenye kichwa tofauti na swali lilivyoulizwa, hivyo walipata alama hafifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika faida za kilimo kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 6.

## UTAMADUNI WA TANZANIA


6. Utamaduni wa Tanzania umebobea katika sekta ya kilimo ambapo kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa, Kilimo kimekuwa ndio chanzo cha maendeleo nchini Tanzania. Ufuatao ni umuhimu wa kilimo nchini Tanzania.

Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa taifa, Tanzania imeweza kupiga hatua katika suala zima la kilimo ambapo taifa linahimiza watu waweze kulima mazao mbalimbali kwani ni chanzo cha kuondoa njaa endapo kama chakula cha kutosha kitakuwepo.

Kilimo huongeza pato la taifa, Tanzania kilimo kimetumika kuongeza pato la taifa kwani mazao mbalimbali yamekuwa yakiuzwa ndani na nje ya nchi hivyo basi pesa hupatikana na kuweza kuongeza pato la nchi kwa namna moja au nyingine.

Kilimo hupunguza umaskini nchini, Tanzania imeweza kusaidia watu mbalimbali kwa kutumia kilimo ambapo maskini wameweza kupungua hivyo basi kama mtu una eneo yakutosha unaweza kupanda chochote kwani kinaweza kukusaidia kwa namna moja au nyingine.

Kilimo ni chanzo cha ajira, watu wamepata ajira sehemu mbalimbali kutokana na kilimo mfano kwenye viwanda ambapo wamekuwa wakichukua malighafi kutoka mashambani na kuweza kupeleka viwandani ili kutengeneza bidhaa mbalimbali, hivyo basi Tanzania inatumia kilimo kama utamaduni wake ili kuweza kupata maendeleo ya nchi.



6. Kilimo ni chanzo cha chakula, Tanzania kumekuwa na uwepo wa chakula cha kutosha kwani kilimo ndio kimepewa kipaumbele na watu hawakosi chakula na hakuna naaja ya njaa nchini Tanzania, hivyo basi utamaduni wa Tanzania ni kilimo.

Kilimo husaidia katika ujenzi wa mundombinu, kupitia utamaduni wa Tanzania ambao ni kilimo barabara zimeweza kujengwa uwanja wa ndege pamoja na barabara za treni ambazo njia zote hizi hutumika katika kusafirisha mazao mbalimbali kwenda ndani na nje ya nchi ya Tanzania.

Hivyo basi kila nchi ina utamaduni wake na Tanzania utamaduni wake ni kilimo ambapo kimekuwa kikitegemewa katika nyanja mbalimbali za uchumi.


**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa faida za kilimo badala ya kuandika kuhusu utamaduni wa Tanzania.

### 2.2.3 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya Maendeleo ya Kiswahili, katika mada ndogo ya Kukua na Kuenea kwa Kiswahili kabla ya Uhuru. Swali lilikuwa mahsusi kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa athibitishe kwa hoja sita mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika utawala wa Waingereza wakati wa ukoloni nchini Tanganyika.

Watahiniwa 19,920 walijibu swali hili, kati yao watahiniwa 19,812 sawa na asilimia 99.5 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata kuanzia alama 6.5 hadi 20 kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. *7:*** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 16,943 sawa na asilimia 85.1 walifanya swali hili, na walipata alama kuanzia 12 hadi 20. Watahiniwa 235 sawa na asilimia 1.2 walipata alama kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kutothibitisha kwa usahihi mambo yaliyosababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza. Watahiniwa wengine walitoa sababu pungufu za kukua na kuenea kwa Kiswahili wakati wa ukoloni, wengine walitoa sababu sahihi lakini walishindwa kuzitetea kikamilifu. Hata hivyo, watahiniwa wachache walitoa hoja sahihi na kuzitetea ipasavyo, hivyo, alama za ufaulu wa watahiniwa wa kundi hili zilitofautiana ingawa wote walifaulu vizuri. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kuwa Kiswahili kilitumika katika shughuli mbalimbali kama vile *shuleni, mahakamani, shughuli za kilimo, utawala na jeshini*. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


7 Kwa kukua na kuenea kwa Kiswahili kuliko
Lugha nyingine za Kimakabila na Kiingereza,
Kusanifisha Kiswahili, Waingereza
walisanifisha Kiswahili kuwa Lugha sanifu mwaka
1925 ambapo gavana wa Tanganyika aliitisha
Mkutano katika nchi zote za Afrika mashariki
Ki kama vile Kenya, uganda na Tanzania
hivyo basi Kiswahili Kilipendekezwa kuwa Lugha
ya Taifa hata baado ya uhuru wa Tanganyika
ambayo ni Tanzania. Hivyo kutokana na kusa
nifisha Kiswahili kilipata idadi kubwa ya
wazungumzaji ukilinganisha na Lugha nyingine
Mfano za Kimakabira, Kiingereza, Kijeremani na
Kiarabu.
Kuchapisha vitabu vya Kiswahili, Wai
ngereza katika utawala wao walichapisha vita
bu kadha wa kadha vilivyoandikwa kwa Lugha
ya Kiswahili ambapo vitabu hivyo vilitumika ka
somo mbalimbali mfano mashuleni shule za
msingi kuanzia darasa la Ina 4 (1-4) pia
Kiswahili kilitumika katika dini ambapo vitabu
kadha wa kadha vya kidini vilichapishwa kwa
ajili ya kuhakikisha kuwa Kiswahili kinasambaa
kutokana na sababu hiyo Kiswahili kilienea
sana kuliko Lugha ambazo hazikuchapishwa
kwenye vitabu mfano Lugha za Kimakabila
Shughuli za manamba (Mashamba), waing
oreza walianzisha mashamba mbalimbali ambapo
watanzania walikuwa wakifanya shughuli za
Kilimo ilikupata chakula na kuepukana na njaa
hivyo basi kutokana na kutojuana kwa hawa
kuweza kuelewana kupitia Lugha zao za

**Kielelezo 7.1**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa katika Swali la 7

Jumla ya watahiniwa 2,869 sawa na asilimia 14.4 walifanya swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Baadhi ya watahiniwa walithibitisha baadhi ya mambo yaliyosaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza kwa usahihi, lakini walishindwa kuelezea mambo mengine. Vile vile, watahiniwa wengine walichanganya mambo yaliyokuza na kueneza Kiswahili kabla ya uhuru na yale ya baada ya uhuru. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi lakini hawakuzitolea ufafanuzi. Udhaifu na ubora wa hoja zilizotolewa na

watahiniwa ulisababisha utofauti wa alama miongoni mwao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile: *(i) Kiswahili kilitumika katika la elimu, (ii) Kiswahili kilitumika shughuli za utawala mfano mahakama, (iii) Kiswahili kilitumika katika suala la manamba.* Hata hivyo, katika kipengele cha (iv)-(vi*)* mtahiniwa alitoa hoja za kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili baada ya uhuru kimakosa mfano*: (iv) kuanzishwa kwa TATAKI (v kutumika kwa Kiswahili katika vyombo vya habari mfano TBC* na *(vi) Kutumika katika bunge la Tanzania*. Majibu hayo yalifanya mtahiniwa apate alama za wastani.

Watahiniwa 108, sawa na asilimia 0.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu. Watahiniwa hao walipata alama 0 mpaka 6. Baadhi ya watahininiwa walieleza hoja za kukua na kuenea kwa Kiswahili wakati wa harakati za kudai uhuru badala ya wakati wa utawala wa Waingereza. Aidha, watahiniwa wengine walitoa hoja zilizo kinyume kabisa, kama vile: *ujenzi wa reli, kuanzishwa kwa vyombo mbalimbali kama TUKI, kutumika kwa Kiswahili katika vyombo vya habari kama TBC na kutumika kama somo chuo kikuu cha Dar es Salaam.* Hivyo, watahiniwa katika kundi hili walitofautiana katika alama zao na walipata alama hafifu. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.




7 KUKUA NA KUENEA KWA LUGHA YA KISWAHILI -ni
hatua na njia ambazo zilitumiwa au kutu
mika ambazo zimefanya kiswahili kuenea na
kukua
Tanganyika ilikua koloni la Waingereza, wakati wa
ukoloni wa Waingereza walitumia njia zifuatazo kuku
za na kueneza Kiswahili
KUJENGA SHULE - Kiswahili kilifundishwa ka
ma somo katika shule za Muingereza, shule hizi
ni zile za Misheni, wanafunzi walisoma kiswahili
kama masomo mengine
KISWAHILI KUWA LUGHA RASMI - Kiswahili kili
fanywa na Waingereza kuwa lugha rasmi ya ma
wasiliano baada ya kiingereza, kwa njia hii Kiswa
hili kilitumika katika uongozi, shule, ofisini
WAINGEREZA KUJIFUNZA KISWAHILI - Waingereza wa
lijifunza lugha ya kiswahili, kurahisisha mawasiliano,
kuongoza watalawa, kwa njia hii Kiswahili kilikuwa
7 KUANZISHA MTAALA RASMI WA KISWAHILI - Mtaala
huu ndio ulitumika mashuleni kufundishia, kuli
andaliwa silabasi maalum ya kufundishia
kiswahili
KUCHAPISHA VITABU VYA KISWAHILI - vitabu
hivi vilitumika mashuleni kufundishia, na pia vili
patikana kwa wananchi kujisomea mf kitabu
cha ushairi wa Fumo Liongo
KUANZISHWA KWA TAASISI YA KISWAHILI - Taa
sisi hii ilijikita katika Isimu ya lugha, ku
soma lugha, kutafiti misamiati mipya ya lugha
Kuchapisha kazi mbali mbali katika lugha ya kiswahili.
Kwa kumalizia napenda kusema kiswahili pia
kilikuwa kwa kukopa misamiati kutoka katika
lugha ya Waingereza mf Organism (English) — Ogani (Swahili)

**Kielelezo Na. 7.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Sahihi katika Swali la 7

### 2.2.4 Swali la 8: Maendeleo ya Kiswahili

Swali lilihusu mada ya Maendeleo ya Kiswahili, mada ndogo ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini baada ya uhuru. Swali lililenga kupima tathmini. Mtahiniwa alitakiwa aeleze kwa hoja sita mchango wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Kulingana na takwimu, watahiniwa 9,639 walijibu swali hili. Watahiniwa 9,178 sawa na asilimia 95.2 walikuwa na ufaulu wa wastani na mzuri kwani walipata alama kuanzia 6.5 hadi 11.5. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali la 8.




**Chati Na.8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Jumla ya watahiniwa 5,152 sawa na asilimia 53.4 walijibu swali hili na kupata alama za juu kuanzia 12 hadi 19. Watahiniwa 64 sawa na asilimia 0.7 walipata alama kuanzia 18 hadi 19 kutokana na sababu mbalimbali. Baadhi ya watahiniwa walibainisha hoja sita lakini hawakuzielezea kikamilifu, watahiniwa wengine walitoa hoja na maelezo sahihi lakini walitoa hoja pungufu. Hata hivyo, watahiniwa wachache walitoa hoja sita zote na kuzielezea kikamilifu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja, kama vile*: (i) kufundisha fasihi na isimu, (ii) kuuza majarida mbalimbali, (iii) kutoa ushauri kwa waandishi chipukizi, (iii) kufanya tafiti katika lugha ya Kiswahili (iv) kutafsiri vitabu vya masomo mbalimbali kwa Kiswahili, (v) kutayarisha walimu na wataalamu wa Kiswahili* na *(vi) Kuchunguza tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kujibu vizuri swali hili.

08. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) hii ni taasisi ambayo inajishughulisha na Uchunguzi wa lugha ya Kiswahili pamoja na Taaluma zake. Taasisi hii mwanzoni ilikuwa Ikiitwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) Lakini pia Tuki baadae ilivunjwa na mnamo mwaka 2009 Ikaanzishwa TATAKI. Taasisi hii Inamchango mkubwa katika ukuaji na Uenezaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Ufuatao ni mchango wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Kuandika Vitabu na Majarida mbali mbali. Taasisi hii Imefanikiwa kuandika vitabu na majarida mbalimbali na Vitabu hivyo huta miwa hata mashuleni na watu mbalimbali wameweza kusoma majarida yao hivyo kutokana na hilo Imechangia kwa kiasi kikubwa kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania.

Imeshirikiana na Taasisi nyingine kama vile BAKITA, BAMITA na taasisi nyingine nyingi katika kuandaa na kuendeleza lugha ya Kiswahili mfano Imeshirikiana na Bamita kutunga mitihani kadhaa hivyo kutokana na hilo taasisi hii Imechangia pakubwa sana katika kukuza na kuendeleza Kiswahili.

Imeandaa warsha na semina mbali mbali. Taasisi hii imetoa semina nyingi mbali mbali kwa lugha ya Kiswahili na katika maeneo tofautitofauti mfano Mashuleni kwa kutokana na semina hizo Imesaidia kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

08. Imetoa miongozo kwa watumiaji wa
lugha ya kiswahili. Taasisi hii Imechangia
kukua na kueneza kwa kiswahili nchini
Tanzania kwani Imefanikiwa kutoa miongozo
mbalimbali kwa watumiaji wa lugha ya kiswa
hili tena hasa kwa wale wanaofundisha
hivyo miongozo, hiyo Imesaidia kukua na
kuenea kwa kiswahili nchini Tanzania.
Imetoa kamusi mbalimbali. Pia
taasisi hii imechangia kukua na kueneza
kiswahili nchini Tanzania kwa kufanikiwa
kutoa na kuchapisha kamusi mbalimbali
ambazo kamusi hizo hutumiwa na watu
ili kuweza kujifunza zaidi lugha ya kiswa
hili na kuangalia maana ya maneno magum
u yaliyopo katika lugha ya kiswahili.
Imefanikiwa kuwatia Moyo kwa
Vijana wanaosoma kiswahili ~~nchi~~ Vyuoni na
Mashuleni. hivyo kutokana na kuwatia
Moyo Vijana hao huweza kusomea
kiswahili mpaka katika ngazi za juu. hivyo
Imechangia katika kukuza na kueneza.
kiswahili nchini Tanzania.
Hivyo; basi TATAKI Imechangia kwa
kiasi kikubwa katika kukuza na kuendeleza
kiswahili nchini Tanzania japo kuwa na changa
moto zinazoikabili Taasisi hii

**Kielelezo 8.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyejibu Vizuri Swali la 8

Halikadhalika, takwimu zinaonesha kuwa, idadi ya watahiniwa waliopata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5 ni 4,026 sawa na asilimia 41.8. Ufaulu huu ulitokana na sababu zifuatazo: Watahiniwa wengine walitathimini hoja chache kwa usahihi na nyingine ambazo hazikutosheleza kuonesha mchango wa Taasisi za Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania, wengine walichanganya mchango wa TATAKI na TUKI, hivyo wakapata alama pungufu. Aidha, baadhi yao walikuwa na hoja chache kwenye kiini,

hawakuwa na utangulizi wala hitimisho kutokana na kukosa maarifa juu ya uandishi wa insha. Hivyo, watahiniwa katika kundi hili walitofautiana katika alama zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa hoja kama vile: *(i) kuchunguza fasihi (ii) kushirikiana na vyama na vyuo vikuu, (iii) kutilia mkazo katika kutumia lugha ya Kiswahili, (iv) kutafsiri vitabu mbalimbali, (v) kukuza maendeleo na matumizi ya Kiswahili fasaha* na *(vi) kutayarisha wataalam wa somo la Kiswahili.* Uchambuzi wa majibu unaonesha kuwa mtahiniwa huyu alishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza.

Pamoja na hayo, watahiniwa 461 sawa na asilimia 4.8 walishindwa kujibu vizuri swali hili, hivyo kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6. Kati ya sababu za ufaulu hafifu kama sababu zifuatazo: kukosa maarifa ya mada ya Maendeleo ya Kiswahili. Watahiniwa wengine walielezea kuhusu idara za TATAKI badala ya mchango wa TATAKI katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Wengine walitoa hoja mbili tu sahihi lakini hawakuwa na utangulizi wala hitimisho, na wachache walitoa changamoto za TATAKI kinyume na matakwa ya swali. Hivyo, watahiniwa hao walitofautiana katika alama zao Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea idara za TUKI katika jibu lake kinyume na matakwa ya swali, kama vile: *(i) idara ya uchapaji, (ii) idara ya fasihi, (iii) idara ya isimu (iv) idara ya kamusi* na *(v) idara ya fashi na istlahi.* Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swali hili.

8. Taasisi ya Taaluma za kiswahili (TATAKI)

Taasisi hushughulika na kukuza na kueneza kiswahili katika nchi ya Tanzania. Zifuatazo ni changamoto zinazoikabili Taasisi hii.

Kutokuwepo kwa fedha za uendeshaji wa Taasisi; Hii inachangia washindwe kuendesha ~~Kibat~~ Virabu mbalimbali za kiswahili katika sehemu za vijijini ambazo zitasaidia kueneza kiswahili kwa haraka na badala yake wat[u] wavijiji bado wanatumia Lugha mama kama Lugha ya mawasiliano.

Kukosekana na wataalamu wa kufundisha wa Lugha ya kiswahili; Hii inachangia na wasomi wengi kuona fahari zaidi kusomea Lugha ya kiingereza na kuiacha Lugha yao, Hivyo kusababisha upungufu wa wataalamu wa Lugha ya kiswahili.

Kukosa utayari wa wajifunzaji; wengi wamini Lugha zao mama kuliko kiswahili hivyo hawana utayari wowote katika kujifunza kiswahili hii ni kutokana na uchache wa watumiaji wa kiswahili huko vijijini ukilinganisha na mjini.

Kutokuwepo kwa sera zinazochochea ujifunzaji na ufundishaji wa kiswahili; Hivyo watu wanatumia Lugha mama au Lugha za kigeni kutokuona umuhimu wa kujifunza kiswahili na kutokukipa kiswahili ulazima katika mawasiliano yao.

Kutumika kwa kiingereza kama Lugha ya kufundishia katika hatua mbalimbali za elimu; mfano sekondari na vyuoni hivyo kufanya watumiaji wa Lugha wasione umuhimu wa Lugha hiyo kwasababu sio Lugha ya kufanyia mtihani au kutokutumika kama Lugha ya mawasiliano wawapo shuleni.

Kukosekana kwa vitendea kazi; kama vile vitabu, matini au machapisho mbalimbali yanayohusiana na Lugha ya kiswahili ili kusaidia kueneza na kukuza kiswahili katika nchi ya Tanzania.

Ili kufanikiwa kukuza na kuenezwa kwa kiswahili serikali inatakiwa itumie kiswahili kama Lugha ya kufundishia katika Ngazi zote za elimu pia waanzishe Taasisi nyingi za kukuza na kueneza kiswahili ambazo zitafika hadi vijijini ili kuwepo kwa uwiano sawa wa watumiaji wa kiswahili.

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Yasiyo Sahihi katika Swali la 8

Kielelezo Na. 8.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu juu ya upungufu katika usanifishaji badala ya mchango wa TATAKI katika kukuza na kueneza Kiswahili.

# 3.0 SEHEMU YA II: KISWAHILI KARATASI YA PILI

Uchambuzi wa takwimu kwa kila swali umefanyika ambapo ufaulu kwa watahiniwa umegawanyika katika makundi matatu ambayo ni ufaulu wa kiwango kizuri, kiwango cha wastani na kiwango hafifu. Sehemu hii itatathmini na kuchambua majibu ya watahiniwa katika mada mbalimbali.

## 3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika karatasi ya pili ya somo hili umegawanyika katika sehemu A na B. Uchambuzi zaidi ulikuwa kama ifuatavyo:


## 3.2 SEHEMU A

Sehemu hii ilitahini maswali manne yenye jumla ya alama 40, na kila swali lilikuwa na alama 10. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu hii.

### 3.2.1 Swali la 1: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi kwa Ujumla, mada ndogo ya Nadharia ya Fasihi. Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa hoja tano umuhimu wa nyimbo za watoto wadogo katika michezo ya watoto. Swali lililenga kupima tathmini.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa wote (20,864) waliofanya mtihani huu. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwani asilimia 96.7 walikuwa na ufaulu wa wastani na mzuri kwa kuwa walipata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na.9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Watahiniwa 16,775 sawa na asilimia 80.4 ya waliofanya swali hili walilijibu vizuri na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 7,726 sawa na asilimia 37 walifanya vizuri zaidi na walipata alama kuanzia 8 hadi 10. Ufaulu wao ulitokana na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya Nadharia ya Fasihi. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa wengine walitoa hoja sahihi lakini hawakuweza kutetea baadhi ya hoja zao ipasavyo. Aidha, baadhi ya watahiniwa walitoa hoja pungufu lakini walizitetea kikamilifu. Watahiniwa wachache waliweza kutoa hoja zote kuhusu umuhimu wa nyimbo za watoto katika michezo ya watoto na walizitetea kikamilifu. Hivyo, alama za ufaulu wa watahiniwa wa kundi hili zilitofautiana. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile: *hukuza utamaduni, watoto hujifunza ujasiri, ushujaa na udadisi, hukuza lugha na huburudisha watoto.* Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri na kupata alama za juu.

1 Nyimbo za watoto ni nyimbo zinazoimbwa na watoto wadogo kwa lengo la kujiburudisha. Ni kweli kuwa Nyimbo za watoto wadogo huwa na umuhimu mkubwa kwa watoto hao. Ufuatao ni umuhimu wa nyimbo za watoto wadogo kwa watoto.

Huburudisha watoto, huu ni mongo ni mwa umuhimu wa nyimbo za watoto kwani watoto huimba nyimbo hizo kwa lengo la kujiburudisha kwa mfano nyimbo inayoimbwa

"Mabata madogo madogo yanaogelea,
yanaogelea, katika shamba zuri
la bustani".

Nyimbo hii watoto huimba kwa sababu huwaburudisha.

Husaidia kutunza kumbukumbu za watoto, pia nyimbo za watoto wadogo katika sanaa za maonyesho ni muhimu kwani huwasaidia watoto kutunza kumbukumbu mbalimbali. Mfano katika nyimbo inayoimbwa

"Sara sara saa ya kwenda kwetu
kwaheri mwalimu, kwaheri mwalimu,
tutaonana kesho.

Katika nyimbo hiyo husaidia watoto kutunza kumbukumbu kwamba ni muda wa kwenda nyumbani umefika.

Husaidia kukuza uelewa wa mtoto, pia nyimbo za watoto zina faida kwa watoto kwani huwasaidia wao

) kukuza uelewa wao. Mfano katika nyimbo inayosema
"Mwalimu wetu apendi kelele,
anapenda nyimbo, na ngelegele."
Hivyo kupitia hii nyimbo inamsaidia mtoto kuelewa kwamba akiwa darasani si vizuri kupiga kelele anatakiwa kukaa kimya.
Hujenga uhusiano mzuri baina ya watoto, pia nyimbo za watoto huwa na faida sana kwani husaidia watoto kujenga uhusiano mzuri miongoni mwao. Hivyo nyimbo za watoto ni muhimu kwani huwasaidia kujenga uhusiano mzuri.
Husaidia watoto kutambua vitu kwa haraka, hii pia ni miongoni mwa faida ya nyimbo za watoto kwa watoto kwani nyimbo huwasaidia wao kutambua vitu kwa haraka mfano
"Hii ndio a, a a a inamkia mrepu
a, a, a,
Hii ndio e, e e e iko kama ngata
e, e e.
Hivyo kupitia nyimbo hiyo humsaidia mtoto kutambua herufi kwa haraka

**Kielelezo Na. 9.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa Yaliyokidhi Matakwa ya Swali

Vile vile, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 3,407 sawa na asilimia 16.3 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Data zinaonesha kuwa tofauti ya alama miongoni mwa watahiniwa wa kundi hili zimesababishwa na mambo yafuatayo: Watahiniwa kushindwa kuelezea kikamilifu umuhimu wa nyimbo za watoto na kushindwa kueleza umuhimu mwingine, watahiniwa wengine walichanganya hoja za umuhimu wa nyimbo za watoto na hoja za umuhimu wa michezo ya watoto. Aidha, wengine hawakuandika utangulizi wala hitimisho katika majibu yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha umuhimu wa nyimbo za watoto kama vile; *hutunza historia ya jamii, huburudisha* na *huongeza ukakamavu.* Hoja hizi zilikuwa sahihi isipokuwa hoja mbili ambazo hazikuwa sahihi, kama vile: *hukaribisha wawekezaji* na *hukuza kilimo.* Hivyo, alipata alama za wastani. Majibu ya watahiniwa hawa yanaonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu nadharia ya Fasihi.

Uchambuzi zaidi wa data unaonesha kuwa, watahiniwa 680 sawa na asilimia 3.3 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Tathmini ya majibu ya watahiniwa wa kundi hili inaonesha kuwa watahiniwa wengi walionesha

wahusika wa fasihi simulizi yaani *wanyama, binadamu, vitu na mahali,* huku wengine wakitoa dhima mbalimbali za fasihi kwa ujumla, kinyume na matakwa ya swali. Kadhalika, watahiniwa wengine walifanikiwa kuonesha dhima chache na kushindwa kutoa baadhi ya dhima kutokana na kukosa maarifa ya kutosha juu ya umuhimu wa nyimbo za watoto wadogo katika michezo ya watoto. Kielelezo Na. 9.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.

Sanaa za maonyesho ni aina ya fasihi simulizi ambayo inahusisha ngonjera, majigambo na aina nyingine nyingi. Nyimbo za watoto wadogo katika sanaa za maonyesho zina umuhimu kwa watoto kupitia hoja zifuatazo;

Fanani; Fanani ni mtu anayewasilisha kazi ya fasihi ambaye husaidia mtunzi katika kupitisha kazi hiyo ambapo huweza kuelimisha, kuburudisha, na kudumisha mila na desturi za jamii, Mfano, Ngonjera.

Hadhira; hadhira husaidia kuonekana kwa sanaa hizo za maonyesho mfano katika ngonjera hadhira lazima awepo ili aweze kusaidia katika kupiga makofi na kushangilia.

Wakati; Sanaa za maonyesho ni lazima ziwe na wakati yaani fasihi lazima iende na wakati kutokana na mabadiliko ya nyanja mbalimbali mfano Televisheni, redio.

Mandhari; Sanaa za maonyesho, hutendeka jukwaani hivyo husaidia kuwepo kwa fanani na hadhira pia mandhari ni muhimu.

Utendekaji; Fanani na hadhira lazima waonyeshe matendo yao kama vile kucheza, kupiga makofi.

Hivyo basi; Sanaa za maoresho zina umuhimu kwa watoto kwani huburudika na kuelimika.


**Kielelezo Na. 9.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na.9.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyeeleza mahitaji ya Sanaa za maonyesho badala ya umuhimu wa nyimbo za watoto wadogo katika michezo ya watoto.

### 3.2.2 Swali la 2: Uhuru wa Mtunzi wa Kazi za Kifasihi

Swali lilitoka katika mada ya Fasihi kwa Ujumla, na mada ndogo ya Uhuru wa Mtunzi wa Kazi za Kifasihi. Swali lilikuwa mahsusi kupima tathmini. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua mambo yanayoonesha kuwa mwandishi wa kazi za kifasihi yuko huru kwa kutoa hoja nne zenye mifano.


Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 20,864 walifanya swali hili. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 18,261 sawa na asilimia 87.5 walipata alama kuanzia 3.5 na 10 kama Chati Na.10 inavyoonesha.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Data katika chati Na.10 zinaonesha kuwa, watahiniwa 15,253 sawa na asilimia 73.1 walikuwa na ufaulu mzuri, kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 7,461 sawa na asilimia 35.8 walifanya vizuri zaidi na kupata alama kuanzia 8 hadi 10, kutokana na sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa waliweza kutaja hoja nne kuonesha mambo yanayoonyesha kuwa mwandishi wa kazi za kifasihi yuko huru, lakini walishindwa kutetea baadhi ya hoja. Watahiniwa wengine waliweza kutoa hoja zote sahihi na kuzifafanua. Kwa mifano, Mtahiniwa mmojawapo aliandika, *kuwa na utashi, kuwa na falsafa moja, aitawale vyema lugha yake na utawala wa*

*Sanaa*. Mtahiniwa pia aliweza kutetea hoja zake kwa usahihi. Kielelezo Na.10.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.


2. Mwandishi kuwa huru ni ile hali ya mwandishi wa kazi ya fasihi kuandaa kazi yake bila kuwa na hofu juu ya tabaka tawala au kuogopa aina yoyote ya changamoto zitakazo mkabili, mambo yanayoonesha kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi yupo huru ni kama yafuatayo.

Uhuru wa mwandishi umo katika utashi mwandishi lazima awe na utashi wake mwenyewe katika kuiandaa kazi yake, bila kulazimishwa na mtu yeyote na hii itaifanya kazi yake ionekane bora zaidi mfano Ngugi wa Thiong na Penina mhando ni baadhi ya waandishi wenye utashi.

Mwandishi lazima aitawale vyema lugha yake ili mwandishi awe huru ni lazima ajue vizuri lugha anayoenda kuitumia na lazima ajue sarufi ya lugha hiyo na ndipo atakuwa huru na kazi yake itakuwa bora na yenye kueleweka zaidi

Mwandishi lazima aitawale vyema sanaa sanaa ni uzuri unaojitokeza katika maumbo tofauti, ili mwandishi awe huru ni lazima aijue na kuitawala vyema sanaa, mfano fasihi kama kipengele kimojawapo cha sanaa, kama mwandishi wa kazi za fasihi lazima atawale vyema fasihi.


Mwandishi lazima awe na falsafa moja inayoeleweka; ili mwandishi awe huru ni lazima awe na imani moja katika kile anachoenda kukiandika; mfano kama imani ya mwandishi ni Mapinduzi ni lazima asimamie imani hiyo bila kuyumbishwa. Mfano Penina mhando katika tamthiliya ya "NGUZO MAMA" ameonesha falsafa yake juu ya ukombozi wa mwanamke hivyo kudhihirisha uhuru wa mwandishi.

**Kielelezo Na. 10.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyejibu Vizuri Swali la 2

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa 3,008 (14.4%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa walichanganya dhima za uhuru wa mwandishi na dhana za uhuru wa mwandishi, lakini wengine walichanganya sifa za mwanafasihi na dhima za uhuru wa mwandishi, kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi mambo kama vile, *mwandishi*

*aitawale vyema lugha yake, mwandishi aitawale vyema sanaa yake na mwandishi awe na falsafa moja inayoeleweka*. Mtahiniwa alitetea hoja zake kwa usahihi lakini alitoa sifa zilizo kinyume na swali, kama vile: *awe mcheshi, awe mchangamfu* na *awe mkarimu* hivyo, alipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 2,603 sawa na asilimia 12.5 walifanya swali hili na walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Miongoni mwa sababu za zilizoathiri ufaulu wa watahiniwa katika kundi hili ni kukosa maarifa juu ya mada ya dhana za uhuru wa mwandishi. Uchambuzi umebainisha kuwa baadhi ya watahiniwa walijibu dhima za uhuru wa mwandishi na wengine dhima za mwanafasihi na kushindwa kukidhi matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijadili mambo manne kama vile: (i) *mandhari, (ii) wahusika, (iii) mada (iv) lengo* kama dhana za uhuru wa mwandishi kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.


2. Uhuru wa mwandishi ni ile hali anayokuwanayo mwandishi kuonesha mambo yote yanayotendeka katika jamii bila kuwa na woga, yafuatayo ni mambo yanoonyesha kuwa mwandishi yuko hulu katika kazi yake.

i/ Mwandishi huonyesha matatizo yote yanoikumba jamii mfano ataonesha, matabaka, Umaskini na Uongozi mbaya

ii/ mwandishi atakuwa huru kuchochea mambo yote wanayofanyiwa tabaka la chini mfano Unyonyaji na Unyanyasaji.

iii/ Mwandishi atakuwa mstari wa mbele kuelimisha jamii juu ya mambo mabaya mfano Uongozi mbaya na rushwa

iii/ mwandishi atatatua matatizo yote yanayoikumba jamii kwa mfano kuanzishwa kwa nyimbo zinazokemea mambo mabaya.


**Kielelezo Na. 10.2**: Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na.10.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu faida ya uhuru wa mwandishi badala ya dhima ya uhuru wa mwandishi.

### 3.2.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi


Swali lilitoka katika mada ya Maendeleo ya Fasihi Simulizi, katika mada ndogo ya Uhifadhi wa Kazi za Fasihi Simulizi, na lililenga kupima uchambuzi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua changamoto tano za njia mbalimbali za kuhifadhi fasihi simulizi.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa 20,684 sawa na asilimia 100 walifanya swali hili. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 19,442 sawa na asilimia 93.2 walipata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na.11 inaonesha viwango vya ufaulu kwa watahiniwa katika swali la 11.




**Chati Na.11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 15,363 sawa na asilimia 73.6 walifaulu kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 7,088 sawa na asilimia 34 walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. watahiniwa hao walichambua kwa usahihi njia za kuhifadhi fasihi simulizi, kama vile, *njia ya kichwa*, *njia ya maandishi, njia ya vinasa sauti, njia ya CD* na *DVD, TEPU* na *njia ya mtandao.* Pia, watahiniwa walichambua changamoto tano za njia hizo za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi. Kielelezo Na. 11.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.



3. i/ Gharama
Kwa mfano katika njia ya vinasa sauti au maandishi, huitaji gharama kikuwezo ku hifadhi fasihi simulizi.

ii/ Muda
Hii ni changamoto kwa mfano njia ya maandishi huchukua muda sana katika uhifadhi wake paka kazi kukamilika hivyo ni changamoto.

iii/ Kupotea kwa haraka na urahisi
Kwa mfano njia ya kichwani, ni rahisi sana kazi ya fasihi kupotea kama mtu anapo sahau, kupotea kumbukumbu na hata kufa, hivyo ni changamoto.

iv/ Kuwamali ya mtu binafsi na kupunguza hadhira
Kwa mfano njia ya maandishi, au vinasa sauti hii hubagua watu wanaojua kusoma na kusikia wengine hutumia hivyo ni changamoto katika uhifadhi.


v/ Kutobadilika kulingana na wakati na kutoku pokea marekebisho pale ambapo kunahitajika. Kwa mfano njia ya maandishi haipokei mabadiliko kulingana na wakati hivyo huyo ni changamoto.

**Kielelezo Na.11.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyekidhi Matakwa ya Swali la 10

Kadhalika, watahiniwa 4,079 sawa na asilimia 19.6 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Uchambuzi wa majibu yao unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa waliweza kuelezea kwa usahihi baadhi ya changamoto za njia za uhifadhi wa fasihi simulizi, lakini walishindwa kueleza njia nyingine, wengine walichanganya faida za njia mbalimbali za kuhifadhi fasihi simulizi na changamoto za kila njia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi changamoto za kuhifadhi fasihi simulizi, kama vile, *kichwani*, *maandishi* na *njia ya mtandao na kompyuta* lakini alielezea changamoto zisizo sahihi za njia za uhifadhi wa fasihi simulizi, kama vile: *Uwepo wa ukoloni mamboleo* na *kukosekana kwa vipaza sauti*. Hii ilipekea kupata alama za wastani. Watahiniwa hawa

wanaonesha kuwa walielewa matakwa ya swali lakini hawakuwa na maarifa ya kutosha, juu ya mada husika.

Uchambuzi zaidi wa data unaonesha kuwa watahiniwa 1,422 sawa na asilimia 6.8 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Sababu za ufaulu huo ni pamoja na: watahiniwa kujibu hoja za umuhimu wa njia mbalimbali za uhifadhi wa fasihi simulizi badala ya changamoto, wengine walichanganya neno changamoto na faida, hivyo, wakachambua faida za njia za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua changamoto tano, kama vile: *huokoa muda, hudumu kwa muda mrefu, huongeza hadhira, huwa mali ya jamii nzima* na *huwasilishwa kirahisi* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali la 10.


3 Fasihi simulizi, ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa njia ya mapokezi ya mdomo, fasihi hii hupata mabadiliko ya papo kwa papo, pia ina fanani na hadhira.

Zifuatazo ni changamoto mbali mbali za kuhifadhi fasihi simulizi.

Uhaba wa vitendea kazi, kwa mfano; majukwaa ya kufanyia kazi ya kuwasilisha kazi hizo

Kutokuwa na kutokujua umuhimu wa kazi ya fasihi, baadhi ya watu hushindwa kuelewa na kujua umuhimu wa kazi ya fasihi hivyo hushindwa kuhifadhi kazi hizo.

Mabadiliko, mara nyingi kazi ya fasihi simulizi hubadilika papo kwa papo kutokana mazingira, hivyo mtu hushindwa kuihifadhi kwa sababu hubadilika badilika.

Tatizo la uwasilishaji, kila mwasilishaji huwasilisha kwa njia yake tofauti tofauti hivyo msikilizaji hushindwa kuelewa kipi na kuhifadhi kipi.

Fasihi andishi, ujio wa fasihi andishi kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yamepeleke watu wengi washindwe kuhifadhi kazi yaote ile ya fasihi simulizi.

Hivyo basi, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yamepeleke watu kushindwa kuhifadhi


**Kielelezo Na. 11.2**: Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na.11.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu matatizo ya uwasilishaji na sifa za fasihi simulizi badala ya changamoto za uhifadhi wa fasihi simulizi.

### 3.2.4 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi


Swali lilikuwa mahsusi kupima uchambuzi na lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi, mada ndogo ya Usanifu wa Maandishi. Swali lilimtaka mtahiniwa kusoma matini aliyopewa kisha kubainisha vipengele kumi vya matumizi ya lugha.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20,864 ambapo watahiniwa 17,431 sawa na asilimia 84.4 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10 kama Chati Na.12 inavyoonesha.




**Chati Na.12**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Chati Na.12 inaonesha kuwa watahiniwa 12,263 sawa na asilimia 58.8 waliojibu swali hili walifanya vizuri na kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya vipengele vya kisanaa katika matini. Miongoni mwao, watahiniwa 5,239 sawa na asilimia 25.1 walipata alama kuanzia 8 hadi 10. Aidha, watahiniwa 576 sawa na asilimia 2.8 walipata alama zote 10 kwa kuwa walibainisha kwa usahihi vipengele vyote kumi vya matumizi ya lugha na walitoa mfano kwa kila kipengele. Kielelezo Na.12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili na kupata alama za juu.



4. i) Mubalagha
Hii ni hali ya kusema jambo kwa kuba chumvi kuliko jambo lenyewe.
Mfano: "Alijaliwa kiuno kikubwa kama mlima Kilimanjaro"

ii) Mdokezo
Hii ni hali ya kusema jambo bila kumalizia, lengo likiwa kumfanya msomaji amalizie kwa maneno yake mwenyewe
Mfano: "Umbea wako nao - - - - - - -"

iii) Tanakali sauti
Hii ni hali ya kuiga sauti au hi mwigo wa sauti jinsi kitu kinavyosikika
Mfano: Tena ..... Chini! Puuu!

iv) Methali
"Mdharau mwiba mguu huota tende"

v) Tashihisi
Hii ni hali ya kuvipa ubinadamu vitu visivyo binadamu sifa za kufanya kama binadamu.
Mfano: "Damu ikaanza kuchunguliia kwenye pua"

4. vi) Tashibiha
Hii ni tamathali ya semi ambayo inalinganisha vitu viwili tofa kwa kutumia viunganishi
Mfano: "Mbilikimo kama nusu pima ya mtu wa kawaida"

vii) Misemo
"Amebugia chumvi nyingi"

viii) Sitiari
Ni tamathali ya semi ambayo hulinganisha vitu viwili tofauti bila matumizi ya kiunganishi.
Mfano: "Sebule likageuka uwanja wa mapambano".


ix) Takriri
Hii ni mbinu ya kurudia maneno ili kuonyesha msisitizo
Mfano: "Watu walijaa, wakajaa, wakajaa"

**Kielelezo Na. 12.1**: Sehemu ya Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa Aliyekidhi Matakwa ya Swali

Takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 5,348 sawa na asilimia 25.6 ya waliofanya mtihani walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi baadhi ya vipengele vya matumizi ya lugha. Aidha, baadhi yao walichanganya vipengele vya lugha na vipengele vya maudhui mfano waliandika vipengele kama, *ujumbe, dhamira* na *falsafa* katika majibu yao. Hata hivyo, mtahiniwa mmoja

alifafanua kwa usahihi vipengele, kama vile: *wahusika, mandhari, matumizi ya taswira, mtindo na muundo* ingawa alitaja vipengele vya ushairi kama vile, *ridhimu, wizani, beti, vina* na *muwala* kimakosa kama vipengele vya matini, hivyo, alipata alama za wastani.

Pamoja na hayo, watahiniwa 3,253 sawa na asilimia 15.6 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Miongoni mwao, watahiniwa 587 sawa na asilimia 2.8 walipata alama 0. Majibu ya watahiniwa hao yalionesha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali na wengine hawakuwa na maarifa ya kutosha. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walibainisha vipengele vya fani badala ya vipengele vya matumizi ya lugha, wengine walifanikiwa kutaja na kueleza kwa usahihi vipengele vichache. Watahiniwa wachache walitaja vipengele bila kuvitolea maelezo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha vipengele vya maudhui kama vile: *(i) msimamo (ii) falsafa (iii) migogoro* na *(iv) maudhui.* Kielelezo Na. 12.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.



4 i. Mtindo
- Mwandishi ametumia mtindo wa maswali na majibu katika kueleza habari hiyo mfano pale anaposema "Na mimi nime sau, ngoja nikumbuke - -"

ii. muundo
- Mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja mfano pale anaposema "Kulikuwa na bwana mmoja jina lake alikuwa anaitwa Kazurura"

iii. Wahusika
- Mwandishi katika habari yake ametumia wahusika mfano Kazurura, marita

iv. Mandhari
- Mwandishi ameyatumia mazingira ya nyumbani na shambani mfano pale anaposema Kazurura humuhimiza mkewe kwenda shambani wakati yeye hubakia nyumbani

v. Ucheshi
- Katika habari hiyo mwandishi ameonyesha ucheshi katika kusimulia kwake habari ambapo humfanya msomaji awe kufurahia mfano pale anaposema "hivi nikuwa nimefika wapi kukusimulia"

4 vi. lugha matumizi ya lugha
- lugha aliyotumia mwandishi ni ngumu kueleweka kwa baadhi ya maneno mfano maneno kama chai ya shira, gonda la fufu hamezi mate

vii. Fani na maudhui
- Ni mambo ambayo yamejadiliwa katika habari hiyo na mwandishi

viii. Taswira
- Mwandishi ameonyesha taswira mbalimbali katika uandishi wake wa habari hiyo

ix. Takriri na Ridhimu
-

x. Lugha ya mkato
- mfano pale anaposema ngoja

**Kielelezo Na.12.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na.12.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye katika kipengele cha (ix) aliandika neno *ridhimu* na kipengele (vii) alibainisha *fani na maudhui* ambavyo ni vipengele vya matumizi ya lugha, kinyume na matakwa ya swali.


## 3.3 SEHEMU B

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu. Swali la tano lilikuwa ni la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60, na kila swali lilikuwa na alama 20.

### 3.3.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi, mada ndogo ya Uhakiki wa Ushairi. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia diwani mbili alizosoma na kutoa hoja tatu kwa kila diwani kutathmini kauli inayosema, "Watunzi wa ushairi huwa na dhima anuai kwa jamii katika kazi zao wanazotunga". Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kufanya tathmini.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wote 20,264 walifanya swali hili. Watahiniwa 20,621 sawa na asilimia 98.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwani walipata alama kuanzia 6.5 hadi 19.5. Chati Na.13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5.




**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Uchambuzi wa matokeo unaonesha kuwa watahiniwa 17,322 sawa na asilimia 83 walijibu vizuri na kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao watahiniwa 887 sawa na asilimia 4.3 walifaulu kwa kiwango kizuri na walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 19.5. Pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa wengi, hakuna mtahiniwa aliyepata alama zote 20 kwa kuwa; baadhi ya watahiniwa walitoa dhima sahihi za ushairi lakini wakashindwa kutetea baadhi ya hoja zao kikamilifu, wengine walitaja hoja pungufu lakini sahihi kutoka katika diwani walizosoma. Aidha, watahiniwa wengine hawakuandika utangulizi wala hitimisho, na wachache waliandika hoja sahihi na kuzitetea ipasavyo, hivyo wakapata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alitaja dhima kama vile: *kuadibu jamii, kutia hamasa jamii na kuhifadhi mila na desturi za jamii*. Katika diwani ya "Mapenzi Bora" alitoa dhima kama vile: *aina za mapenzi bora, sifa za mapenzi bora*, *faida za mapenzi bora* na kuzielezea kwa kina. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hawa walielewa mahitaji ya swali na walikuwa na ujuzi wa kufanya tathmini, hususani katika kazi ya ushairi. Kielelezo Na. 13. kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali.


5. Watunzi wa ushairi ni watu wanaojiu bughulisha katika utungaji wa mashairi mbalimbali. Ni kweli kuwa watunzi wa ushairi huwa na dhima anuai kwa jamii katika kazi zao wanazozitunga. Kwa kutumia diwani ya CHUNGU TAMU iliyoandikwa na Theobald Mvungi na KIMBUNGA iliyoandikwa na Haji G. Haji zifuatazo ndizo dhima za watunzi wa ushairi katika jamii.

Kwa kuanza na diwani ya CHUNGU TAMU zifuatazo ndizo dhima anuai za watunzi wa ushairi kwa jamii:-

Kukosoa jamii. Watunzi wa ushairi huwa na dhima ya kukosoa jamii yaani kudhibitisha maovu yapatikanayo katika jamii ili kuirekebisha jamii kwamfano; shairi la "Chini ya mti mkavu":-

"Tulio wengi twajua, hawa wanaotudhulumu
Chakula kutumezea, kwa niaba ya kaumu
Kwa maringo watembea, matumbo yenye karamu
Lakini yajulikana, kuwa tu haitoshi" Mtunzi wa shairi anaikosoa jamii kwa kuonesha jinsi viongozi waliopo madarakani wanavyotumia mali za umma kwa manufaa yao.

Kuhimiza jamii iachane na matabaka. Watunzi wa ushairi wana dhima ya kusisitiza jamii iachane na matabaka ili kukuza umoja na ushirikiano baina ya watu katika jamii kwamfano; shairi la "Wimbo wake hotubani"



5 "Punda na yule ngamia
Wanajua kuvumilia
Hata njia ya siku mia
Lakini siku zikiwadia
Vituo watavijua" Mtunzi wa ushairi anahimiza juu ya suala la kukandamiza tatizo la matabaka baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa.

Kupiga vita usaliti baina ya wanandoa. Watunzi wa ushairi huwa na dhima ya kupiga vita tatizo la usaliti linalojitokeza miongoni mwa wanandoa wengi katika jamii. Kwa mfano; shairi la "Fikra za Waungwana"
"Ana unanichukia, si ajabu hunitaki
Sijui nilokosea, kwako mimi sipendeki
Jusufu ndo wamjua, wampenda kwa malaki
Ana wangu wa nyumbani, sema nakusikiliza"
Watunzi wa ushairi wanapiga vita tatizo hili ili kuzuia uvunjifu wa ndoa nyingi katika jamii.

Kwa kumalizia na diwani ya KIMBUNGA iliyoandikwa na Haji G. Haji zifuatazo ndizo dhima anuai za watunzi wa ushairi kwa jamii:-

Kuasa jamii iachane na rushwa. Watunzi wa ushairi huwa na dhima ya kuiasa jamii iachane na rushwa kwani ni tatizo lililokithiri sana katika jamii na ambalo huyumbisha maendeleo ya jamii. Kwa mfano; shairi la "Rushwa":-
"Rushwa kajenga kambi, na kuondoka hataki
Afanya kila vitimbi, mkaidi hashindiki

**Kielelezo Na.13.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyefanya Vizuri Swali la 5

Uchanbuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 3,299 sawa na asilimia 15.8 walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Majibu yao yalionesha kuwa, baadhi walishindwa kutoa maelezo sahihi kwa baadhi ya dhima za watunzi wa ushairi, wengine walichanganya dhima za watunzi na dhamira za vitabu husika. Vile vile, watahiniwa wengine walitaja dhima sahihi za watunzi wa ushairi lakini maelezo yao hayakutosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Chungu Tamu" alitoa dhima za watunzi kama vile: *kuelimisha jamii, kuburudisha jamii na kuhifadhi mila na tamaduni za jamii*. Katika diwani ya "Kimbunga" mtahiniwa akatoa

dhamira kama vile*: usaliti, unafiki na matabaka.* Mtahiniwa huyo alichanganya dhima na dhamira hivyo, alipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 243 sawa na asilimia 1.2 walijibu vibaya swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6. Alama za watahiniwa katika kundi hili zilikuwa hafifu kwa sababu baadhi yao walijadili dhamira badala ya dhima za watunzi kama vile: *Rushwa, matabaka na Umuhimu wa kazi* kutoka katika diwani ya "Kimbunga". Katika diwani ya "Fungate ya Uhuru" alitathmini hoja kama vile: *wizi, usaliti* na *uzalendo*. Pia, wengine walitoa hoja chache, na wachache walitaja dhima za ushairi bila kuzitolea maelezo. Kielelezo Na.13.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili kwa kushindwa kukidhi matakwa ya swali.

5 Watunzi wa Ushairi; Ni watu ambao hujishughulisha na Utungaji wa Mashairi na kuyasambaza katika sehemu husika kwa Malengo tofauti tofauti. Ni kweli kuwa kwamba Watunzi wa Mashairi huwa na dhima zao anuai wanazo tunga na dhima hiyo kubwa ni kufikisha ujumbe uliopo. Kwa kutumia diwani ya FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMED S. KHATIBU na diwani ya KIMBUNGA iliyoandikwa na HAJI GORA.

Kwa kuanza na diwani ya KIMBUNGA ambayo imeonesha jinsi watunzi wa Ushairi huwa na dhima anuai katika jamii.


Rushwa ni kikwazo cha Maendeleo katika jamii; hii ni dhima ambayo watunzi huielezea katika jamii kuwa suala rushwa ni tatizo kubwa sana hasa katika kufikia maendeleo Mwandishi au Mtunzi anaeleza katika shairi lala la "rushwa" anasema

"Rushwa kajenga kambi, kuondoka hataki
afanya kila vitimbi, mkaidi ashindiki"

Uwepo wa Matabaka ni chanzo cha kudidimiza Maendeleo; Pia Watunzi wanajitahidi kutoa dhima zao kwa kuikumbusha jamii kwamba katika jamii fulani pange kuwepo na Matabaka basi Maendeleo lazima yawe hafifu kwa maana kutakuwa hakuna Ushirikiano mtunzi ameeleza katika shairi la "Wenye vyao watubana" Mtunzi anasema

"Wenye vyao watubana lakutanyiza hatuna
lakutanyiza hatuna tusaumia Maskini
Wakubwa tuteteeni wenye vyao watubana"

Ufanyaji mzuri wa kazi ni sehemu ya kufanikisha Malengo; Watunzi wanazidi kutoa dhima yao anuai kwa kuikumbusha jamii kuwa ni lazima uwajibike katika kutaka kufikia Malengo yao Mfano Mwandishi anaeleza katika shairi la "KAZI" anasema " Pesa huletwa na kazi ni njia upitayo
Uache uvivu wako"



5 Kwa kumaliza na diwani ya FUNGATE YA UHURU ambayo imetea tathmini ya ukweli huo kama ifuatavyo

Wizi ni kikwazo cha maendeleo katika jamii; pia watunzi wa ushairi mbalimbali wanaeleza jamii kuwa suala la kuchukua kitu au vitu vya watu bila ruksa ni tatizo kwa sababu huweza kukwamisha maendeleo ya mwingine. Mtunzi ameeleza suala la wizi katika shairi lake la "Wizi" anasema

"Wizi umo
Makanisani
Misikitini".

Suala la usaliti ni kikwazo katika jamii; jamii yeyote ambayo inataka kufikia malengo basi ni vyema ikapiga vita usaliti kwa sababu suala hilo la usaliti linaweza kupelekea matabaka katika jamii. Mtunzi ameeleza katika shairi lake la Tumesalitiwa anasema

"Nikate tamaa?
Kwani twendako hatufiki
Mambo yaliyo ni unafiki
Tumesalitiwa.

Uzalendo ni jambo muhimu katika jamii; hii ni kwa sababu ili jamii iweze kufikia malengo yake ni vyema kila raia awe na upendo katika nchi yake. Mtunzi ameliónesha hilo katika shairi la "Nchi yangu" ambalo huonesha mtu aliyeo na mapenzi ya dhati na nchi yake anasema

"Nchi yangu naipenda
naipenda ntakufa naipenda".

Kwa hiyo: watunzi wa ushairi katika jamii yeyote huwa na lengo lao katika kuandaa kazi hizo na miongoni mwa dhima hizo ni kutoa jumbe mbalimbali katika jamii zao.

**Kielelezo Na.13.2:** Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu Swali la 5


Kielelezo Na.13.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu dhamira za vitabu badala ya dhima za watunzi wa ushairi.

### 3.3.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi

Swali hili lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi, katika mada ndogo ya Uhakiki wa Ushairi. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha kufaa kwa masuluhisho mbalimbali yaliyopendekezwa na washairi kuhusu changamoto zinazokabili suala la mapenzi na ndoa katika jamii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu. Swali lilikuwa mahsusi kupima uchambuzi.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa na watahiniwa wachache (3,032). Idadi hiyo ni sawa na asilimia 14.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa Kiswahili. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa

asilimia 68.1 ya watahiniwa walipata alama kuanzia 6.5 hadi 18.5 kama Chati Na. 14 inavyoonesha.





**Chati Na. 14**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 987 sawa na asilimia 32.5 walijibu vizuri swali hili na kupata alama kuanzia alama 12 hadi 18.5. Watahiniwa 11 sawa na asilimia 0.1 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa walipata kuanzia alama 18 hadi 18.5. Pamoja na ufaulu wa juu, watahiniwa hao walishindwa kupata alama zote 20 kwa kuwa baadhi ya masuluhisho waliyotoa hayakuwa sahihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika, *ili kupunguza migogoro ya ndoa oa wake zaidi ya mmoja*. Hoja hizo si sehemu ya mapendekezo yaliyotolewa na washairi. Watahiniwa wachache walitoa masuluhisho stahiki kulingana na washairi hivyo walipata alama 18.5. Kielelezo Na.14.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

6. Mapenzi na ndoa; Hii inamaanisha ya watu kuwa na mahusiano katika maisha yao ambayo hufanya kuwa na familia. Mapenzi na ndoa katika jamii huwa na sehemu kuu mbili ambazo ni mapenzi ya dhati na mapenzi yasiyo ya dhati. Hivyo basi kufuatana na masuluhisho tisho mbalimbali yaliyopendekezwa na washairi kuhusu changamoto zinazokabili suala la mapenzi na ndoa katika jamii. Kuonesha na upungufu wa aina mbalimbali ambao lazima kufuatwa kwa kutumia vitabu viwili vya ushairi ~~kitabu~~ ya CHUNGU TAMU iliyoandikwa na ~~Theobald~~ THEOBALD A. MVUNGI pamoja na diwani ya Fungate ya uhuru FUNGATE YA UHURU iliyoandikwa na MOHAMMED S. KHATIBU katika kuonesha mafunzo yanayohitajika katika mapenzi na ndoa.

Suala la mapenzi na ndoa waachiwe watu wawili wanaopendana; Mwandishi wa diwani hii ya Chungu tamu anatoa suluhisho kwa kutumia mashairi ya Thomasi na Dotto namna walivyokuwa wanapendana katika shairi la Thomasi na Dotto kuhusu mapenzi, yao yaliingiliwa na watu wengine ambao ni wazazi wao likapelekea kuvunjika. Hivyo basi ili pawepo/pawezekane kuwepo na mapenzi ya na ndoa za kweli lazima kuachwa watu wanaopendana.

Usaliti katika mapenzi na ndoa hupelekea ndoa kukosa furaha katika jamii. Hii ni suluhisho ambalo mwandishi wa diwani ya chungu tamu ameeleza kuonyesha kwa watu wakuu na wazazi katika ndoa zao wanawezesha kujenga jamii iliyo na mapenzi na ndoa za kweli. Mwandishi ameonesha katika shairi la fikra za wanawake akionesha namna mwanamke alivyoweza kukaa ameni ya ndoa yake baada ya kuwa na mwanaume mwingine.



**Kielelezo Na. 14.1**: Majibu ya Mtahiniwa Aliyekidhi Matakwa ya Swali

Watahiniwa 1,079 sawa na asilimia 35.5 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Ufaulu huo ulisababishwa na baadhi ya watahiniwa kuelezea kwa usahihi baadhi ya masuluhisho ya changamoto za mapenzi. Watahiniwa wengine walitoa changamoto sahihi lakini walishindwa kutetea baadhi ya masuluhisho. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya "Chungu Tamu" alijibu kwa usahihi hoja, kama vile: *Katika mapenzi kuna kukubaliwa na kukataliwa, imani potofu huvuruga mapenzi na ndoa, Suala la mapenzi waachiwe wawili wapendanao.* Katika diwani ya "Kimbunga", mtahiniwa alielezea dhamira badala ya masuluhisho, kama vile: *dhuluma, maonyo na maadili na udereva.* Hivyo, alipata alama za wastani.

Vile vile, watahiniwa 966 sawa na asilimia 31.9 walipata alama hafifu, kuanzia 0 hadi 6. Watahiniwa wachache (0.2%) walishindwa kuonesha baadhi ya masuluhisho ya changamoto zinazokabili suala la mapenzi na ndoa katika jamii na badala yake walijadili dhamira katika diwani hizo. Wengine walieleza vipengele vya fani katika ushairi, kama vile, *muundo, mtindo, wahusika* na *mandhari*. Kielelezo Na.14.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili, hivyo kupata alama hafifu.

6. Masuluhisho, Ni kitendo cha kusuluhisha
mambo mbalimbali au migogoro mbalimbali inayojitokeza katika
jamii zetu, Ni kupli kwa washairi hujaa kwa masuluhisho
kuhusu changamoto zinazokabili suala la mapenzi na ndoa
katika jamii. kwa kutumia diwani mbili ambazo ni
"FUNGATE YA UHURU" iliyoandikwa na Mohamed MOHAMED
S. KHATIBU pamoja na diwani ya "KIMBUNGA" iliyoandikwa
"HAJI GORA HAJI." Kwa kuanza na diwani ya "kimbunga"
yafuatayo ni masuluhisho yanayotumiwa na washairi ili kuondoa
changamoto zinazoikabili suala la Mapenzi katika jamii.

Kupiga vita rushwa, washairi huondoa mapenzi.
changamoto zinazoikabili mapenzi na ndoa, kwa sababu mwandishi
hupiga vita rushwa katika jamii. kwa sababu katika suala
zima la rushwa linakuwa lina pelekea kutoendelea kijamii,
mwandishi anasuluhisho changamoto hii kwa kutumia
shairi la "RUSHWA'. Hivyo basi wale wote wanaopokea rushwa
hawafai kuingwa katika jamii zetu.

Kupiga vita wizi na udokozi, mwandishi husuluhisha
changamoto za wizi na udogozi udokozi katika jamii
kwa kuwahasa viongozi wote wanaojihusisha na udokozi pia
moja na wizi wa mali ya umma waweze kuacha mara moja
na badala yake mali hizo zitumike katika kujenga jamii
mpya. hata kuonyo jamii za kiafrika kuna baadhi ya watu na
viongozi wanakuwa wanaiba mali za umma kwa ajiri ya manufaa
yao binafsi. Mwandishi anaeleza haya katika shairi la
"PARA"

Kupiga vita umbea, Mwandishi huyaondoa matatizo
yote yanayoikumba mapenzi na doa katika jamii kwa kuishauri
jamii iweze kuepukana na umbea na majukeo yake jamii
iweze kujishughulisha na shughuli mbalimbali ambazo zina
weza kuleta maendeleo katika jamii zetu mwandi-
shi anasisitiza haya katika shairi la "WACHA HAYO"

**Kielelezo Na.14.2**: Sampuli ya Majibu Yasiyo Stahili Swali la 6


Kielelezo Na.14.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu dhamira mbalimbali za ushairi badala ya masuluhisho ya washairi juu ya mapenzi na ndoa.

### 3.3.3 Swali la 7: Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka kwenye mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi andishi katika mada ndogo ya Uhakiki wa Riwaya. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja nne kwa kila kitabu kutoka vitabu viwili vya riwaya alivyosoma. kuthibitisha kauli isemayo “Mkulima mzuri hujua matatizo ya shamba lake na mwandishi mzuri hujua matatizo ya jamii yake”.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20.833 sawa na asilimia 99.9. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri zaidi ukilinganisha na maswali mengine katika mtihani kwa sababu ambapo watahiniwa 20,781 sawa na asilimia

99.8 walipata alama kuanzia 6.5 hadi 19.5. Chati Na.15 inaonesha viwango vya ufaulu kwa watahiniwa kiasilimia.





**Chati Na.15:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 15*

Watahiniwa 323, sawa na asilimia 1.6 walifanya vizuri swali hili hivyo walipata kuanzia alama 18 hadi 19.5. Takwimu zinaonesha kuwa, pamoja na watahiniwa kufanya vizuri swali hili, hakuna mtahiniwa aliyepata alama zote 20, kutokana na sababu zifuatazo: badala ya kutoa hoja nne kwa kila kitabu, walitoa hoja tatu na kuzielezea kwa kina. Watahiniwa wengine hawakuandika hitimisho katika kazi yao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja nne sahihi kwa kutumia riwaya ya "Usiku Utakapokwisha", kama vile: *tatizo la matabaka, tatizo la umasikini* na *tatizo la usafiri.* Aidha, katika riwaya ya "Mfadhili" alifafanua matatizo kama vile: *uzembe kazini*, *Tatizo la ulevi*, *Tatizo la mapenzi na ndoa* na *tatizo la usaliti*. Mtahiniwa aliweza pia kutoa hitimisho linaloendana na swali. Kielelezo Na.15.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

7. Matatizo ni mambo mabaya ambayo husababisha kutokuwa na maendeleo. Ni kweli kwamba Mkulima Mzuri hujua matatizo ya shamba lake na Mwandishi mzuri hujua matatizo ya jamii yake. Hii huthibitishwa kwa kufuemia riwaya mbili ambazo ni VUTA N'KUVUTE iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi pamoja na riwaya ya MFADHILI iliyoandikwa na Hussein Tuwa. Waandishi hawa wanajadili matatizo mbalimbali kwa kuanza na riwaya ya VUTA N'KUVUTE.

Tatizo la mila potofu. hii ni moja ya matatizo ambayo huikumba jamii zetu ambapo mwandishi anamuonesha Yasmini ambaye anakumbwa na tatizo hilo ambapo wazazi wake wanaendeleza mila ya kumchagulia mtoto wao mchumba ambaye ni mzee (Bwana Raza) hivyo inampelekea Yasmin kushindwa kukaa na Bwana Raza na mwisho anaamua kutoroka; hivyo hata katika jamii zetu mambo kama haya yapo hivyo jamii ij iepukane na mambo hayo ili kuweza kuleta maendeleo.

Tatizo la Matabaka. pia katika riwaya hii mwandishi anaziungumzia suala la matabaka ambapo linakuwa na tabaka la chini ambalo ni akina Denge, Mwajuma na Mambo, pia tabaka la juu ambapo ni Inspekta wright pamoja na Kopro matata hii inapelekea kutokuwepo na maendeleo Pia hata katika jamii zetu kuna jamii nyingi ambazo zinaendeleza matabaka hivyo tuepukane na matabaka ili kuleta maendeleo.


7 Tatizo la rushwa; katika riwaya
hii mwandishi anazungumzia suala la
rushwa ambalo limetumiwa tatizo, pale amba
po Koplo Matata anaonekana kumpa
Yasmin rushwa ili aweze kupatafika
habari za Denge lakini Yasmin anakataa.
Hata katika jamii zetu kuna baadhi ya
viongozi ambao huendeleza rushwa hivyo
jamii inatakiwa kuepukana na rushwa ili
kuweza kuleta maendeleo.
Tatizo la usaliti; katika riwaya
hii suala la usaliti linaonekana pale
ambapo Koplo Matata anaonekana kuwa
Saliti kwa kuwapiga wenzake na kushirikiana
na Inspekta Wright ambaye ni mkoloni
hii ~~inatata~~ inawapoteza watu kupigania
hali zao, hivyo hata katika jamii zetu
kuna watu ambao huwasaliti wenzao na
kushirikiana na watu wabaya hivyo tuepu
kana na usaliti ili kuleta maendeleo.

**Kielelezo Na.15.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama za Juu

Vile vile uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa 715 (3.5%) ya waliofanya swali hili walipata alama za wastani, kuanzia 6.5 hadi 11.5. Watahiniwa katika kundi hilo walipata alama hizo kutokana na sababu zifuatazo: Watahiniwa wachache walitoa maelezo ambayo baadhi yalijitosheleza lakini mengine hayakujitosheleza katia kujibu swali. Watahiniwa wengine walitoa sifa za mwandishi bora, na wengine walionesha kwa usahihi matatizo ya jamii yanayoibuliwa na waandishi bora katika jamii zao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika riwaya ya “Mfadhili” alitoa sifa za msanii, kama vile: *awe anaifahamu jamii yake, ajue historia ya jamii yake, ajue lugha ya jamii yake* na *ajue utamaduni wa jamii yake.* Lakini katika riwaya ya “Kufikirika” mtahiniwa alieleza kwa usahihi matatizo ya jamii kama vile: *Uongozi mbaya, madhara ya kafara ya damu, ugumba na utasa* na *suala la Imani potofu katika jamii,* hivyo, akapata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa (52) sawa na asilimia 0.2 walishindwa kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama hafifu kuanzia alama 0 hadi 6. Baadhi ya watahiniwa walijadili aina za mapenzi na ndoa huku wengine walijadili matatizo ya mashamba, kama vile, *magugu, ukame, wanyama waharibifu, tatizo la mbegu* na *ukosefu wa mbolea* bila kuhusisha hoja na vitabu walivyosoma. Kielelezo Na.15.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

07 . Mwandishi ni mtu yoyote anayejishughuli
sha na Utunzaji na Uandishi wa kazi ya
fasihi na kutoa hisia zake kwa jamii ku
pitia njia ya Mazungumzo kwa kutumia
riwaya ndoto ya NAFADHALI iliyoandikwa
na HUSSEIN TUWA na VUTA N'KUVUTE iliyoa
ndikwa na SHAFI ADAM SHAFI. kwa kuanzia na
riwaya ya NAFADHALI
Mgogoro kati ya Bi. Hanuna kwa Dania
Mgogoro huu ni wa kijamii chanzo chake ni
Dania kuamua kumsaliti Gaddi kwa kuzaliana
na Jerry baba yake junior. suluhisho Bi. Han
una kujenga chuki kwa Dania. Suala kama hili
lipo katika jamii zetu za kiafrika watu
Wamekuwa wakiweka chuki kwa watu
kwa sababu ya kuwatenda ndugu zao
wanaowapenda. Mwandishi ameonyesha saba
bu ya Bi. Hanuni kumchukia Dania.
Mgogoro kati ya Gaddi Bullah na
Jerry. Mgogoro ni wakijamii chanzo chake ni
Jerry kumdanganya Dania amuache ili waweze
kumlea Mtoto wao junior kama wazazi wote
wawili. Suluhisho ni Gaddi kuamua kuwaacha
Waendelee na Mahusiano yao kama kawaida.
Watu kama Gaddi katika jamii wapo
wanafanya vitu na kuamua japo kina wauma
za moyo lakini wanaamua kupambana wao
ili kujiepusha na Mambo hatarishi.
Mgogoro kati ya Nunu na Jerry
Mgogoro huu pia ni Wakijamii, chanzo chake
ni Jerry kumshawishi Dania amwache Gaddi
ili aweze kuridiana nae na kuendelea na

07 suala lao la kulea Mtoto wao wakiwa pamoja
Suluhisho Dania kumchukia Jerry kwa kum
shawishi Ujinga Dania. Nunu aliweka chuki
kwa Jerry kwa sababu Jerry alimsababishia
Matatizo. Watu wanaofanya vitu kama Jerry
wapo wengi sana kwa jamii zetu wamek
uwa wakisababisha Mahusiano ya watu
kuvunjika huku wao wakifurahia kwa Matatizo
hayo.


Kielelezo Na. 15.2: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyefanya Vibaya Swali la 7

Kielelezo Na.15.2 ni sampuli ya mtahiniwa aliyeeleza migogoro mbalimbali katika riwaya badala ya matatizo yanayoibuliwa na wasanii katika jamii.

### 3.3.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya

Swali hili lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi, katika mada ndogo ya Uhakiki wa Tamthiliya. Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kwa mifano namna kipengele cha majibizano kilivyosaidia kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya na kuwa nyenzo ya kufikisha ujumbe wa mwandishi. Mtahiniwa alitakiwa kutumia tamthiliya mbili alizosoma, na kutoa hoja tatu kwa kila kitabu. Swali lililenga kupima tathmini.

Jumla ya watahiniwa 17,635 sawa na asilimia 84,5 walifanya swali hili. Watahiniwa 16,653 sawa na asilimia 94.4 walifaulu vizuri kwani walipata alama kuanzia 6.5 hadi 19.5. Chati Na.16 inaonesha bayana viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16.




**Chati Na.16**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 16*

Takwimu katika chati Na.16 zinaonesha kuwa, watahiniwa 14,777 sawa na asilimia 83.8 walikuwa na ufaulu mzuri kwani walipata alama kuanzia 12 hadi 19.5. Watahiniwa 652, sawa na asilimia 3.8 walifaulu vizuri zaidi kwa kupata alama kuanzia 18 hadi 19.5 kwa kuwa waliweza kutumia hoja tatu kwa kila kitabu kuthibitisha namna kipengele cha majibizano kilivyosaidia

kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya na kuwa nyenzo ya kufikisha ujumbe katika tamthiliya mbili walizosoma. Hata hivyo, watahinwa walishindwa kupata alama zote kutokana na sababu zifuatazo: watahiniwa wachache waliweza kuonesha majibizano ya wahusika lakini walichanganya baadhi ya wahusika na vitabu vyao. Kwa mfano, mhusika *Mtolewa* kuwekwa katika kitabu cha *‘‘*Morani” badala ya kitabu cha “Kivuli kinaishi”. Watahiniwa wengine walitoa hoja pungufu japo walizielezea kwa kina, huku wachache wakitoa hoja na maelezo sahihi kulingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya “Kwenye Ukingo wa Thim” alionesha majibizano baina ya *Mzee* na *George*, *Pasta* na *Martha* na *Stella* na *Martha*. Pia, katika tamthiliya ya Morani alionesha majibizano baina ya *Malongo*, *mzee* na *mapoto, Hadikwa* na *Dongo* na *Jalia, Mlemeta* na *Yusufu,* na akaonesha namna majibizano hayo yanavyopendezesha lugha na kutoa ujumbe wa mwandishi. Kielelezo Na.16.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 8.


8. Majibizano ni hali au kitendo cha watu zaidi ya mmoja kuongea kwa kupokezana. Ujumbe ni mambo ambayo msomaji wa kazi ya fasihi huweza kuyapata. Ni kweli kwamba kipengele cha majibizano husaidia katika kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya na kuwa nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wa Mwandishi katika Tamthiliya; kwa kutumia Vitabu ~~vya~~ cha KIVULI KINAISHI kilicho andikwa na ~~Emmanuel Bongo na kitabu cha~~ Said Mohamed na kitabu cha MORANI kilichoandikwa na Emmanueli mbogo. Kipengele hiki kimesaidia kama ifuatavyo. Kwa kuanza na kitabu cha KIVULI KINAISHI amejadili:-

8 'Majibizano kati ya Bi Kizee na watoto;
Mwandishi ametumia majibizano hayo katika
kupendezesha kazi hii na kufikisha ujumbe wa
kuwa jasiri ni mhimu katika kuleta maende-
leo ambapo ~~Kizee~~ Bi Kizee anawasimulia
watoto historia ya Giningi ambayo ilikuwa
ni ya kuogopesha mfano Bi Kizee: watakuwa--
na Watoto:- wako wapi --- (Wananong'ona). Hivyo basi
hata katika jamii yetu mambo hayo yapo.
Majibizano kati ya Mtolewa na Bawabu II.
Mwandishi ametumia majibizano hayo kuleta
ujumbe wa kwamba suala la rushwa halipaswi
katika ujenzi wa maendeleo. Ambapo mtolewa
anaombwa na Bawabu II kutoa rushwa ili kusudi
aweze kuingia ndani ya Kijiji cha Giningi
na aliweza kutoa shilingi elefu tano. Hata katika
jamii zetu mambo haya yapo.
Majibizano kati~~ke~~ ya ~~Fatan~~ Mtolewa na ~~Nyangurungu~~ Bi Kirembwe;
Mwandishi amejadili majibizano hayo kupitia
wahusika hao ambapo ameibua ujumbe wa
kujiamini na kuwa mzalendo ni jambo la busara ~~ka~~
katika kupambana na uhujumu uchumi. Ambapo
Nungunungu "anasema" tumenunue huyu" naye
Jalia anauliza kwa kusema" nani mnunue?".
Hata katika jamii zetu mambo hayo yapo. Kwa

**Kielelezo Na. 16.1**: Sampuli ya Sehemu ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyejibu Vizuri Swali la 8

Aidha, watahiniwa 1,876 sawa na asilimia 10.6 walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kwa sababu zifuatazo: baadhi ya watahiniwa walitoa majibu sahihi na mengine yasiyo sahihi. Watahiniwa wengine hawakuandika utangulizi wala hitimisho katika kazi zao, na wachache walijadili migogoro badala ya majibizano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika tamthiliya ya "Kivuli kinaishi" alijadili migogoro kama vile: *mgogoro kati ya wenye nacho* na *wasionacho, mgogoro wa kimapenzi kati ya Aisha* na *Nungunungu* na *mgogoro kati ya Jalia* na *Mlemeta* na *Yusufu*. Mtahiniwa huyu alienda kinyume na matakwa ya swali hivyo, alipata alama za wastani.

Halikadhalika, watahiniwa 982, sawa na asilimia 5.6 waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6. Watahiniwa hawa walishindwa kutumia hoja tatu kwa kila kitabu kutoka tamthiliya mbili walizosoma kuthibitisha namna kipengele cha majibizano kinavyosaidia kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya na kuwa nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Watahiniwa wachache walijadili majibizano ya wahusika wachache na wengine walitaja tu majibizano bila kuyatolea ufafanuzi, kinyume na matakwa ya swali. Hivyo, walipata alama hafifu. Kielelezo Na.16.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali la 8.



8 Migogoro:- ni hali ya kukinzana baina ya pande mbili au zaidi. Kuna migogoro ya aina nne migogoro ya kinafsi, migogoro ya kijamii, migogoro ya kiuchumi na migogoro ya kiutamaduni. Migogoro ni sawa na majibizano hivyo husaidia kujenga na kupendezesha kazi ya tamthiliya. Kwakutumia tamthiliya mbili nathibitisha kauli hiyo. Tamthiliya ambazo ni Morani na Nguzo Mama. Nikianza na tamthiliya ya "NGUZO MAMA" mwandishi Penina Muhando naonesha jinsi migogoro ilivyotokea.

Mgogoro kati ya Chizi na Bi tatu:- Mgogoro huu ulikuwa unahusu usaliti wa Bi Tatu ambae ni Shangazi yake Chizi kumsaliti na kumkana kuwa yeye si ndugu yake wala Shangazi yake. Tunaona jinsi Chizi alivyokuwa akijibizana na Bi Tatu akimwambia wewe ni shangazi yangu lakini Bi Tatu alikataa na kumwambia kuwa atamfungulia mbwa hivyo aondoke aende zake.

Mgogoro kati ya Bi Tano na wanakikundi wenzake:- Hapa tunaona jinsi Bi Tano alivyokuwa akigombana na kujibizana na wenzake kuhusu swala la Utambaa, Bi Tano alishindwa kuuza utambaa na kundi nayo ndipo wenzake wakaanza kumwambia kuwa uvivu ni umemtawala Bi Tano ndipo wanakikundi wakaamua kugawana utambaa na kila mtu kuenda kuuza sehemu yake.

Mgogoro kati ya Bi Saba na Shemeji zake:- Mgogoro huu ulitokea baada ya kifo cha mumewake Bi Saba. Bi Saba alinyimwa kuendesha na kupewa mali alizochuma na marehemu mume wake baada ya kifo cha Mumewe. Tunaona jinsi mashemeji zake Bi Saba walivyochukua mali

8 zote ikiwemo vyombo, vitanda, makochi hata hivyo waliamua kuchukua hadi watoto. Hivyo Bi Saba aliweza kudhulumiwa mali za marehemu mume wake na mashemeji zake.

**Kielelezo Na.16.2**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyepata Alama Hafifu

Kielelezo Na.16.2 ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu migogoro ya wahusika katika tamthiliya badala ya majibizano ya wahusika na kuonesha namna yanavyopendezesha na kufikisha ujumbe wa mwandishi.

## 4.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada zote kumi na moja (11).

Ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2021 umeongezeka katika mada zifuatazo: Riwaya (99.8%), Utungaji (98.1%), Tafsiri na Ukalimani (96.9%), Tamthiliya (94.4%), Fasihi kwa Ujumla (90.5%) na Usanifu wa Maandishi (84.4%) ikilinganishwa na ule wa mwaka 2020 ambapo ufaulu katika mada hizo ulikuwa kama ifuatavyo: Riwaya (99.4%), Utungaji (97.2%), Tafsiri na Ukalimani (69.7%), Tamthiliya (36.5%), Fasihi kwa Ujumla (70.2%) na Usanifu wa Maandishi (58%).

Aidha, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2021 umepungua katika mada za Ufahamu na Ufupisho (99.5%), Maendeleo ya Kiswahili (97.4%), Utumizi wa Lugha (90.1), Ushairi (83.4%), na Matumizi ya Sarufi (83.1%) ikilinganishwa na mwaka 2020 ambapo kiwango cha ufaulu wa mada kilikuwa: Ufahamu na Ufupisho (99.6%), Maendeleo ya Kiswahili (99%), Utumizi wa Lugha (95%), Ushairi (86.3%), na Matumizi ya Sarufi (98.5%). Ijapokuwa muachano wa mada hizi kati ya mwaka 2020 na 2021 ni mdogo, Mada ya Matumizi ya Sarufi imekuwa na muachano mkubwa zaidi kwani ufaulu wa mwaka 2021 umeshuka kwa asilimia 15.4, ikilinganishwa na mwaka 2020.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mada zote kwa mwaka 2021 ulikuwa mzuri ukilinganishwa na mwaka 2020 hivyo, asilimia 100 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Watahiniwa wengi walikuwa na ufaulu mzuri kwa mwaka 2021 kutokana na sababu zifuatazo: uelewa wa kutosha kuhusu mada zote zilizotahiniwa, matumizi sahihi ya lugha na uzingatiaji wa alama zote za uandishi, uzingatiaji wa matakwa ya swali, kutoa hoja sahihi zenye mifano thabiti.

## 5.0 HITIMISHO

Taarifa hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2021 kilikuwa kizuri kwani asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu. Ufaulu katika mada zote ulikuwa mzuri. Ufaulu mzuri umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa, ujuzi na weledi wa mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha ufaulu wa watahiniwa kimefanana na kiwango cha ufaulu cha mwaka 2020, ambapo watahiniwa walikuwa na ufaulu wa asilimia 100.

Uchambuzi uliofanyika unaonesha kuwa, watahiniwa walifanya vizuri sana mtihani wa somo hili la Kiswahili kutokana na sababu kama vile: kujibu kulingana na mahitaji ya swali, uelewa mkubwa wa mahitaji ya swali, mada kuu na mada ndogo, uwezo mkubwa katika kujibu maswali na kutetea hoja kwa mifano bayana.

## 6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ufaulu wa somo la Kiswahili ni mzuri kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na wadau wengine wa elimu. Hivyo, ili somo hili liendelee kuwa na ufaulu huo, yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie mbinu ya midahalo, mijadala, makongamano kama mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji ambazo zitawaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa zaidi.

(b) Walimu wawaongoze wanafunzi kufanya ziara za kimasomo ili kujifunza kwa vitendo katika maeneo mbalimbali.

(c) Walimu watumie njia ya maswali na majibu, bungua bongo na vielelezo wakati wa ujifunzaji ili watahiniwa wajifunze kwa vitendo.

(d) Walimu wawahimize wanafunzi kusoma vitabu vya kiada na ziada na majarida/machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada zote ili wawe wabobezi zaidi katika ujifunzaji.

*Kiambatisho A*

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2021**

| Na. | Mada | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa waliopata wastani wa 35% ya alama au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Riwaya | 1 | 99.8 | Vizuri |
| 2. | Ufahamu na Ufupisho | 1 | 99.5 | Vizuri |
| 3. | Utungaji | 1 | 98.1 | Vizuri |
| 4. | Maendeleo ya Kiswahili | 2 | 97.4 | Vizuri |
| 5. | Tafsiri na Ukalimani | 1 | 96.9 | Vizuri |
| 6. | Tamthiliya | 1 | 94.4 | Vizuri |
| 7. | Fasihi kwa Ujumla | 3 | 90.5 | Vizuri |
| 8. | Utumizi wa Lugha | 1 | 90.1 | Vizuri |
| 9. | Usanifu wa Maandishi | 1 | 84.4 | Vizuri |
| 10. | Ushairi | 2 | 83.4 | Vizuri |
| 11. | Matumizi ya Sarufi | 2 | 83.1 | Vizuri |

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2021**

